UCHANGANUZI WA NAMNA BURHANI ANAVYOTATUA MATATIZO YANAYOKABILI JAMII KATIKA RIWAYA ZAKE

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY

NA
ROTICH PETER KIBET

Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya Uzamili (M.A KISWAHILI) ya Idara ya Lugha na Isimu ya Chuo Kikuu Cha Egerton

EULIB
068775

JUNI 2005

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kikuu chochote.

ROTICH P.K _____ SAHIHI _____ 06.07.05 TAREHE

IDHINI

Tasnifu hii imeidhinishwa na sisi kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Egerton:

1. DR. BEJA S.K _____ SAHIHI _____ 06/07/05 TAREHE

2. DR. FURAHA CHAI _____ SAHIHI _____ 06-07-05 TAREHE

HAKI ZA NAKILI

© ROTICH P.K 2005

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupigisha chapa au kutafsiri tasnifu hii kwa namna yoyote ile bila idhini kutoka mtafiti au Chuo Kikuu Cha Egerton.

SHUKRANI

Kwanza, ninatoa shukrani kwa Mola kwa kunipa afya njema iliyoniwezesha kusoma na kushughulikia utafiti huu bila shida yoyote hadi nilipohitimu shahada yangu ya Uzamili. Pili, ningependa kuwashukuru wasimamizi wangu: Dr. S.K Beja na Dr. Furaha Chai. Walijitolea kunisaidia kwa ushauri na kunielekeza jinsi ya kushughulikia utafiti wangu. Ninawashukuru pia wahadhiri wengine katika idara ya Lugha na Isimu ambao walinihimiza na kunitia moyo wakati nilikuwa nikifanya utafiti huu, hawa ni Dr. Onyango na mwalimu Mayaka.

Ninawashukuru pia wanafunzi wenzangu katika darasa la M.A (2003-2005) waliokubali kunichangia mawazo kuhusu mada yangu. Hawa ni; Sangolo J.A na Owala S.O. Sitawasahau pia walimu walionipa msingi katika lugha ya Kiswahili na Fasihi; Kidato cha kwanza hadi nne – Dr Ngome, na kidato cha tano na sita - Bw. Cherutoi, Bw. Kachila na Bw. Zalo. Katika Chuo Kikuu cha Nairobi nilipofanyia sahada yangu ya kwanza, ninawashukuru walimu wangu walionipa maarifa zaidi katika uwanja wa Kiswahili, hawa ni kama vile; marehemu Prof. Kitsao, Dr. Wamitila, Dr. Timammy, Dr. Habwe na Dr. Omboga.

Sitasahau aila yangu; mke wangu Lucy na watoto wangu kwa kuvumilia, kujinyima na kunipa moyo wa kuendelea na masomo yangu hadi nilipomaliza. Shukrani za kipekee zinamwendea mamangu, Leah C. Rotich ambaye alinisomesha hadi nikapata kazi na kuweza kujikimu. Ninawashukuru pia dadangu Mary na mumewe Dr. Chepchieng kwa usaidizi wa kipekee niliopata kutoka kwao kila mara nilipokuja Chuo Kikuu cha Egerton kwa masomo yangu. Aidha ninawashukuru dada zangu, Sr. Teresia na Ann ambao walinisaidia kwa njia moja ama nyingine na kunipa uwezo wa kustahimili magumu yaliyoambatana na kazi hii.

Mwisho, ninatoa shukrani za kipekee kwa walionisaidia katika kupiga chapa kazi hii, hawa ni Macca na Chepsiror na wengine ambao ingawa sikuwataja kwa majina walinisaidia kwa njia moja ama nyingine. Ninawaombea wote baraka za Mwenyezi Mungu, niliowataja na wale ambao sikuwataja.

TABARUKU

Ninaitabarukia aila yangu, mke wangu Lucy na wanangu: Brigid, Brenda, Bruce, Caren, Scholar na Kelvin.

ABSTRACT

Human society is always faced with problems, which come with diverse conflicts. So as to regain harmony and peace, members of a society are forced to look for a solution and ways to resolve their problems. Novelists, Burhani being one of them portray this state of affairs in their writings. The novels of Burhani have not been analyzed much, however, this research dealt with how the writer resolves the problems he exposes in his novels. The research critically analyzed the novels of Burhani: *Mali ya Maskini* (1981) and *Mwisho wa Kosa* (1987). The research analyzed the problems facing the society exposed in these novels and how the writer resolves them.

In methodology, the type of research used was content analysis in the collection of data and non-descriptive qualitative analysis in the analysis of data. The results of the research proved that Burhani has exposed diverse problems facing the society and recommends ways of resolving them. The problems he exposes are for instance, poverty, corruption, hatred and harassment of women in marriage. In resolving them, Burhani recommends various ways in, for example, identifying the problem, discussing it, mediation and co-opting the weaker party. When the above ways failed, Burhani recommends the use of jails and courts. This research has exposed the kind of problems Burhani exposes and how he resolves them. It will also encourage future researchers to expose more about Burhani as a writer and his novels.

INKISIRI

Jumuiya ya binadamu daima haikosi kuwa na matatizo ambayo huambatana na migongano ya aina mbalimbali. Ili kuishi maisha yenye amani na salama binadamu hutafuta mikakati ya kutatua matatizo yake. Waandishi wa riwaya, Burhani akiwa mmoja wao, husawiri hali hii katika kazi zao. Riwaya za Burhani hazijashughulikiwa sana na utafiti huu ulilenga kubainisha namna anavyosawiri hali hiyo. Utafiti ulichanganua riwaya za Burhani; *Mali ya Maskini* (1981) na *Mwisho wa Kosa* (1987). Ulichanganua namna ambavyo Burhani anatatua matatizo ya jamii anayoyamulika katika riwaya zake. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa ni kuthibitisha mambo mawili. Kwanza ni kwamba, Burhani amemulika matatizo mbalimbali katika riwaya zake, yaani hakujifunga katika matatizo ya namna moja. Pili, ilikuwa ni kubainisha mikakati mbalimbali aliyotumia katika utatuzi wa matatizo hayo. Kwa sababu matatizo yote yaliyomulikwa yamejengeka katika migongano ya namna mbalimbali, utafiti huu ulizingatia nadharia ya mgongano ambayo iliasisiwa na Karl Marx na mikakati iliyopendekezwa na wanasosiolojia ya kuondoa migongano inayozushwa na matatizo hayo.

Katika utafiti huu nilitumia utaratibu wa upekuzi wa yaliyomo katika ukusanyaji wa deta. Katika uchanganuzi wa deta, utafiti ulitumia mbinu ya kithamano ambapo nilichanganua deta ya matukio yanayodhihirisha matatizo na namna ambavyo mwandishi anatumia mikakati mbalimbali katika juhudi za kuondoa matatizo hayo. Matokeo ya utafiti huu yaliweza kuthibitisha kuwa, Burhani amemulika matatizo mbalimbali yanayoikabili jamii, kama vile; umaskini, mkengeuko, ufisadi, kudhibitiwa kwa mwanamke katika ndoa na chuki. Pili, amependekeza mikakati mbalimbali katika utatuzi wa matatizo hayo, kama vile; kutambua tatizo, kulizungumzia tatizo, kushauriana na kupatana. Mikakati hiyo ilipokosa kufaulu, asasi za jela na mahakama zilitumika. Utafiti huu ulifichua mengi kuhusu matatizo anayoyamulika Burhani katika jamii. Aidha utafiti huu utawachochea watafiti wa siku za usoni wafichue zaidi kuhusu Burhani kama mwandishi na riwaya zake.

YALIYOMO

Ungamo .....(i)
Kibali ..... (i)
Haki za Nakili.....(ii)
Shukrani..... ...(iii)
Tabaruku.....(iv)
Inkisiri ....(v)
Yaliyomo .....(vi)

SURA YA KWANZA
UTANGULIZI.....1
1.0 Utangulizi.....1
1.1 Usuli wa Mada 1
1.2 Mada ya Utafiti 3
1.3 Madhumuni ya Utafiti 3
1.4 Nadharia Tete 4
1.5 Umuhimu/Natija ya Utafiti 4
1.6 Upeo wa Utafiti.....4

SURA YA PILI
YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA.....7
2.0 Utangulizi.....7
2.1 Maandiko Kutoka Nje ya Kenya.....7
2.2 Riwaya za Kiswahili.....9
2.3 Misingi ya Nadharia.....17
2.3.1 Nadharia ya Mgongano 17
2.3.2 Migongano Mbalimbali.....21
2.3.2.1 Utawala wa Mabwana.....21

2.3.2.2 Miji Kama Uwanja wa Mgongano.....22
2.3.2.3 Mkengeuko na Mpisho.....23
2.3.2.4 Elimu.....24
2.3.2.5 Aila (Familia).....24
2.3.2.6 Uana.....26
2.3.2.7 Dini.....28
2.3.2.8 Usawa wa Kijamii.....28
2.3.3 Mikakati ya Kuondoa Mgongano.....29

SURA YA TATU
MBINU ZA UTAFITI.....31
3.0 Utangulizi.....31
3.1 Ukusanyaji wa Deta.....31
3.2 Uchanganuzi wa deta 32

SURA YA NNE.
MATATIZO YANAYOMULIKWA NA NAMNA YANAVYOTATULIWA.....35
4.0 Utangulizi.....35
4.1 Matatizo Yanayomulikwa Katika Kila Riwaya.....36
4.1.1 *Mali ya Maskini*.....36
4.1.1.1 Umaskini na Chanzo Chake.....36
4.1.1.2 Mkengeuko na uhuru wa Vijana.....38
4.1.1.3 Matumizi Mabaya ya Mamlaka.....41
4.1.1.4 Wivu na Chuki Katika Familia.....43
4.1.2 *Mwisho wa Kosa*.....45
4.1.2.1 Mkengeuko na Madhara Yake.....46
4.1.2.1.1 Kuasi Utamaduni.....47
4.1.2.1.2 Matumizi ya Madawa ya Kulevya.....49
4.1.2.2 Ufisadi.....51

4.1.2.2.1 Ulaji Rushwa.....51
4.1.2.2.2 Matumizi Mabaya ya Mamlaka.....52
4.1.2.3 Kudhibitiwa kwa Mwanamke katika Ndoa.....53
4.1.2.4 Wivu, Chuki na Uhasama 55
4.2 Namna Burhani Anavyotatua Matatizo Yaliyomulikwa.....57
4.2.1 Kutambua Tatizo 57
4.2.2 Kulizungumzia Tatizo 58
4.2.3 Kustahimili 59
4.2.4 Mashauriano na Mapatano 60
4.2.5 Kufaana na Kufadhiliana.....61
4.2.6 Asasi za Jela na Mahakama.....62

SURA YA TANO

HITIMISHO.....63
5.0 Utangulizi.....63
5.1 Matokeo ya Utafiti.....64
5.2 Matatizo Yaliyokumba Utafiti.....66
5.3 Mapendekezo.....66

MAREJELEO.....67

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.0 Utangulizi

Tasnifu hii ni utafiti katika uwanja wa fasihi. Ni kazi ya uhakiki katika utanzu wa riwaya. Riwaya zilizochanganuliwa ni za Z.Burhani: *Mali ya Maskini* (1981) na *Mwisho wa Kosa* (1987). Utafiti ulihusu uchanganuzi wa matatizo yanayokabili jamii kama yanavyomulikwa katika riwaya za Burhani na namna ambavyo anatumia mikakati mbalimbali kutatua matatizo hayo. Mpaka sasa, riwaya za Burhani hazijatafitiwa Kwa kiwango ambacho riwaya za waandishi wengine WA riwaya za Kiswahili zimetafitiwa. Riwaya za wasanii kama vile M.S Mohamed, E.Kezilahabi, Shaaban Robert, S.A Shafi miongoni mwa wengine zimetafitiwa kwa pakubwa, mathalani, katika tafiti kama vile za Mlacha (1985 na 1986), Senkoro (1982 na 1987), Shija (1975), Njogu na Chimera (1999) na Njogu (1997). Swali iwapo waandishi hawa wanatoa suluhisho au la kwa matatizo ya jamii wanayoyamulika katika kazi zao limejibiwa katika baadhi ya tahakiki hizo. Aina za matatizo na namna wanavyoyatatua imedhihirika. Utafiti huu kwa hivyo unafichua namna ambavyo Burhani anatatua matatizo ambayo anayamulika katika riwaya zake.

1.1 Usuli wa Mada

Wanariwaya, kama wasanii wengine wa fasihi hutumia fasihi kusawiri hali halisia katika jamii na katika kufanya hivyo humulika masuala nyeti na matatizo yanayowakabili wanajamii na kupendekeza njia za kutatua matatizo hayo. Fasihi kama kioo cha jamii, kwa hivyo tunaweza kuona jamii katika uhalisia wake katika kazi za kisanaa. Matatizo yanapotokea, huibuka hali ya mtafaruku na migongano miongoni mwa wanajamii; migongano hiyo inapofikia kilele, suluhisho hutafutwa ili kuondoa matatizo hayo.

Barani Afrika kuna matatizo ya aina mbalimbali katika nyanja zote za kimaisha; siasa, uchumi utamaduni, kijamii na kadhalika. Kutokana na matatizo hayo, kunaibuka

migongano ya namna mbalimbali na migongano hiyo inapofikia kiwango cha kutovumilika, suluhisho hutafutwa.

Burhani amesawiri hali hii japo anaegemea upande wa mahusiano ya kijamii-kitamaduni na kwa kiasi matabaka na uchumi. Kila penye tatizo hapakosi kuwepo na mgongano. Katika fasihi, mgongano ni muhimu sana katika kuendeleza na kuyakinisha maudhui. Kwa hivyo katika utafiti huu, nilirejelea matatizo yaliyojengeka katika migongano ya namna mbalimbali, migongano hiyo inavyofikia kilele na namna ambavyo Burhani anatoa suluhisho kwa kila tatizo.

Kilele ni sehemu muhimu sana katika kazi ya sanaa kwani hapo ndipo inabainika kama mwandishi anatoa suluhisho kwa matatizo yanayokabili jamii au la. Msokile, M (1993:36) anajadili umuhimu wa kilele katika kazi ya fasihi. Anasema kuwa hii ni sehemu ambayo kwayo, inatarajiwa haja za wasomaji hukidhiwa. Ndipo ambapo jibu muhimu la fasihi hupatikana; jibu ambalo pengine limecheleweshwa na mbinu-rejeshi au taharuki. Aghalabu, kilele hutokea mwishoni mwa kazi ya hadithi, hata hivyo, si lazima kilele kiwe hivyo,na si lazima kiwe kimoja tu-Panaweza kuwa na vilele vingi ama hata ikatokea kusiwe na kilele kabisa katika kazi hiyo ya fasihi. Aidha, kuna kilele aina mbili; kilele cha juu na kilele cha chini (mpomoko). Kilele cha juu ni ambapo suluhisho hupatikana ilhali kilele cha chini ama mpomoko ni ambapo matazamio ya hadhira hayakidhiwi, hali hii inaweza kutokana na udhaifu wa msanii au maksudi ya mwandishi. Utafiti huu kwa hivyo ulifaa ili kudhihirisha kazi za Burhani kama zinatoa suluhisho kwa matatizo ya jamii au la. Aidha ulibainisha matatizo anayoyamulika na namna anavyotumia mikakati mahsusi kutatua matatizo hayo.

Kazi hii ni ya uhakiki na mwishoni mwa utafiti, itaweza kudhihirisha kama Burhani alifaulu au katika kufichua matatizo yanayokabili jamii na kupendekeza suluhisho la kutegemewa. Msokile (1993:10) anajadili kuhusu dhima na wajibu wa mhakiki. Anasisitiza kuwa mhakiki anayo dhima kubwa ya kuamua ubora wa kazi ya sanaa na hivyo kutamka kiwango kilichofikiwa cha maandishi yanayohusika. Katika utafiti huu, tathmini ilifanywa kuhusu kiwango ambacho Burhani kama mwandishi amefanikiwa katika kusawiri jamii katika uhalisia wake; wanajamii wakiwa katika harakati zao za kupambana na mazingira ili kupata afueni. Aidha, matatizo yanayokabili

jamii yaliyomulikwa katika riwaya za Burhani yalijadiliwa na mikakati anayopendekeza itumiwe katika utatuzi wa matatizo hayo.

Senkoro, (1982) anaelezea kuhusu maudhui katika kazi ya fasihi na tahakiki. Anasema migongano ina umuhimu katika kukamilisha kazi ya kisanii na ni sharti msanii ajiulize, migongano aichunguzayo ina umuhimu gani katika maisha ya jamii? Mafunzo, falsafa na maadili yaibushwayo na uchambuzi wa migongano hiyo una nafasi gani katika maendeleo ya jamii? Yamtukuza na kumtetea nani? Yanampinga nani? Baada ya hapo, uhalisi wa maudhui unachunguzwa, ikiwa yale anayoyazungumzia msanii yanalandana na maisha na mazingira ya jamii au sehemu ya jamii inayohusika? Maswali hayo ya Senkoro yalikuwa muhimu sana katika kazi hii. Utafiti huu ulienda hatua moja zaidi na kupambanua matatizo yanayovyazwa na migongano hiyo na mikakati anayotumia mwandishi katika kuyatatua. Tuliona kuwa Burhani ni mwandishi anayezingatia uhalisia wa maisha katika jamii. Anayamulika matatizo yanayokabili jamii na kupendekeza njia za kutatua kwa namna inayowapa matumaini wasomaji wake.

1.2 **Mada ya Utafiti**

Utafiti ulichanganua riwaya za Burhani, namna ambavyo anatatua matatizo yanayokabili jamii. Matatizo yanayakabili jamii anayoyamulika Burhani katika riwaya zake na namna anavyotumia mikakati mbalimbali kuyatatua haijulikani. Utafiti ulijikita katika riwaya zake; *Mali ya Maskini*, *Mwisho wa Kosa*. Riwaya hizi za Burhani hazijashughulikiwa sana. Utafiti ulifichua aina za matatizo anayoyamulika Burhani na mikakati anayopendekeza zitumiwe katika utatuzi wa matatizo hayo.

1.3 **Madhumuni ya utafiti.**

(i) Kupambanua matatizo yanayokabili jamii ambayo Burhani anayamulika katika riwaya zake.

(ii) Kubainisha mikakati inayopendekezwa na Burhani na namna anavyoitumia katika juhudi za kutatua matatizo katika jamii.

1.4 **Nadharia Tete.**

(i) Burhani amemulika matatizo yanayokabili jamii katika riwaya zake.

(ii) Burhani ametumia mikakati mbalimbali katika juhudi za kutatua matatizo katika jamii katika riwaya zake.

1.5 **Umuhimu/Natija ya Utafiti.**

Utafiti huu ni nyongeza katika hazina ya tafiti za kifasihi hasa kuhusu namna wasanii wanavyotatua matatizo katika jamii katika riwaya zao. Watafiti waliotangulia wamechanganua riwaya za Shaaban Robert, Shafi Adam Shafi, S.A Mohamed miongoni mwa wengine na kuonyesha iwapo waandishi hawa wanachangia kwa njia yoyote katika utatuzi wa matatizo katika jamii ama wanakwepa jukumu hilo.

Pili, utafiti huu ulidhihirisha namna ambavyo Burhani anayatatua matatizo yanayokabili jamii katika riwaya zake. Watafiti kama vile Kimani Njogu (1997) na Njogu na Chimera (1999) wameonyesha namna ambavyo wanariwaya wengine wamemulika na kutatua matatizo katika jamii chini ya tawala za kiimla. Kwa mfano, S.A Mohamed, M.S Mohamed, S.A.Shafi, George Orwel miongoni mwa wengine. Katika utafiti wao wameonyesha namna mageuzo makali ama mapinduzi yanatekelezwa ili kutatua matatizo katika jamii. Burhani kwa upande wake anapendekeza njia zisizohasiri mtu yeyote bali kuleta mapatano na kuwapa waathiriwa fursa ya kuanza upya baada ya kukiri makosa yao.

Tatu, utafiti utawafaa watafiti wa siku za usoni katika uwanja wa fasihi, hasa riwaya za Burhani. Riwaya za Burhani hazijashughulikiwa kwa mapana kama riwaya za wasanii wengine wa fasihi ya Kiswahili. Ninatumaini kazi hii itawatia hamu watafiti wengine wafichue mambo mengi mapya kuhusu Burhani kama mwanariwaya na riwaya zake.

1.6 **Upeo wa Utafiti**

Utafiti huu ulichanganua matatizo mbalimbali yanayomulikwa katika riwaya za Burhani na namna ambavyo anayatatua. Utafiti ulijihusisha na matukio yanayodhihirisha matatizo na juhudi za wahusika katika kutatua matatizo hayo. Matukio hayo yapo katika vipera mbalimbali vya mahusiano ya kijamii kama vile

kitamaduni, kiuana, kiumri, kiaila, na kadhalika. Katika uchanganuzi wa kila aina ya tatizo, tulionyesha vile ambavyo mwandishi anawawekea wahusika wake mikakati mbalimbali ili kutatua tatizo hilo.

Utafiti huu uliwahusisha katika uchanganuzi wahusika wanaotumiwa na mwandishi ili kutekeleza dhamira zake. Mwandishi anaweza kuwaumba na kuwajenga wahusika kwa njia mahsusi ili kuweza kumulika matatizo fulani katika jamii na kupendekeza njia za kuweza kuyatatua matatizo hayo. Katika riwaya za Burhani, usawiri wa wahusika ulikuwa muhimu sana katika kutuelekeza kwa matukio ambayo tuliyatumia katika kazi hii. Tulirejelea hulka za wahusika kwa kupata ushahidi kupitia; usemi wao, matendo yao, yanayosemwa na wahusika wengine kuwahusu, na maelezo ya mwandishi kuwahusu. Crysyal, (1987) anatoa baadhi ya maelezo hayo kama njia ya kupata ushahidi kutoka uumbaji wa wahusika katika riwaya. Anasema;

> '...wahusika katika riwaya waweza kujengwa kwa namna mbalimbali.Msanii anaweza kuwaeleza kwa njia ya moja kwa moja;wahusika wengine waweza kuzungumza juu yao-na wanaweza kujizungumzia...'(uk77) (Tafsiri yangu)

Kwa hivyo, utafiti huu ulijikita katika matatizo yanayomulikwa na mwandishi na mikakati wanayotumia wahusika wake ili kutatua matatizo hayo. Kwa kiasi kikubwa, kazi hii imechanganua maudhui, hata hivyo, haikurejelea maudhui yote ambayo yalijitokeza bali yale yaliyoonyesha matatizo katika jamii na namna yanavyotatuliwa. Wasanii wengi wametolewa nakisi kwa kuandika kazi zao bila kuisaidia jamii kwa kupendekeza mikakati ya kutatua matatizo yanayokabili jamii ili kuyafanya maisha ya wanajamii kuwa bora zaidi. Kuna
waandishi wanaojadili matatizo chungu nzima lakini kazi zao zinamalizikia taharuki ama utamaushi, yaani hali ya kukata tamaa badala ya kuleta matumaini. Mathalani, Kezilahabi katika riwaya zake: *Kichwamaji, Dunia Uwanja wa Fujo* na *Rosa Mistika.* Burhani kwa upande mwingine amejitokeza kama mwandishi anayewapa wanajamii matumaini; kwamba japo mambo yamemwendea mrama mhusika fulani, anaweza akaanza upya iwapo atakiri kosa lake.

Utafiti huu kwa hivyo, ulijikita tu katika matatizo yaliyomulikwa katika riwaya za Burhani na namna ambavyo mwandishi anafaulu katika kutumia mikakati

mbalimbali kutatua matatizo hayo. Uchanganuzi ulifanywa katika riwaya moja baada ya nyingine. Katika mbinu za utafiti, utafiti ulitumia utaratibu wa upekuzi wa yaliyomo katika ukusanyaji wa deta na mbinu ya kithamano katika uchanganuzi wa deta.

SURA YA PILI

YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

2.0 Utangulizi

Sehemu hii itajadili baadhi ya maandiko ambayo yamewahi kuandikwa kuhusu mada. Kuna sehemu mbili; maandiko kutoka nje ya Kenya na maandiko katika riwaya za Kiswahili. Sehemu hii inajadili tahakiki za watafiti wa awali katika utanzu wa riwaya, hasa waliochanganua matatizo na migongano katika jamii na namna wasanii wanapendekeza matatizo hayo yatatuliwe. Aidha misingi ya nadharia imejadiliwa, ikiwa nadharia ya mgongano. Nadharia hii iliteuliwa kwa sababu mada ya utafiti inahusu matatizo na utatuzi wa matatizo hayo. Matatizo hujengeka katika migongano; migongano hiyo inapokua na kufikia kiwango cha kutovumilika na mtu ama kundi fulani katika jamii kuathiriwa, kunatokea haja ya kutafuta suluhisho. Kwa hivyo nadharia itakuwa katika sehemu mbili kuu; migongano katika nyanja mbalimbali ya kijamii na matatizo yanayoibuka na juhudi zinazotumiwa ili kuondoa migongano na kutatua matatizo hayo.

2.1 Maandiko Kutoka Nje Ya Kenya

Roger, (1977) anajadili kuhusu wahusika na matendo yao katika kazi ya hadithi. Utafiti huu ulitumia matukio kama deta, matukio ambayo yanatokana na matendo na usawiri wa wahusika. Roger anaeleza kuwa mwanariwaya ana mtazamo na msimamo maalum wa wahusika wake katika mkururo wa mahusiano. Rai hii inaona mwandishi kama anayeelekeza na kuamua matendo na matukio ya wahusika, usawiri na sifa zao zote. Anaeleza na kuamua yeye mwenyewe. Mtazamo huu wa Roger ulifaa sana katika utafiti huu kwani Burhani amewaumba wahusika wake kihalisia; matendo yao na matukio ni yakinifu. Wanapokabiliwa na matatizo, wanajitahidi kuyatatua na kuyaondoa.

Forster (1962) alichangia sana utanzu wa riwaya. Alibainisha aina mbili za wahusika katika riwaya-wahusika bapa na wahusika duara. Anaeleza kuwa wahusika walioumbwa kwa ubapa hujieleza katika sentensi moja kwa mfano Caleb Balderstone

katika *The Bridge of Lammemoor* ni mhusika ambaye hatumii kishazi kamili lakini kinaweza kumweleza sawasawa.

Mhusika huyu haishi nje yake, hana uchu, tamaa au hata ustaarabu unaomfanya kuwa kigeugeu. Kila anachofanya, kote anakoenda, uongo wowote anaousema au sahani anazozivunja ni kwa dhamiri ya kuficha umaskini wa nyumba ya mkubwa wake. Hali hii ni mgongano wa kinafsia kwa sababu mhusika huyu anajizuia ili asije akafichua udhaifu wa mkubwa wake. Kwa upande mwingine, Forster anaeleza kuwa wahusika duara ni wahusika wenye uwezo wa kustaajabisha. Mathalani wahusika wakuu katika *War and Peace*, baadhi ya wahusika wa *Proust* na wote katika *Dostoyersky*. Kwa mfano mtumwa mkongwe wa familia, Duchess wa Guarmantees, M de Charlus na Sain Loup; Madame Bavary, ambaye kama Mall Flonders anaitawala riwaya yake na pia anaweza kupanua na kufumbua bila upinzani wowote. Aidha, riwaya zingine alizoshughulikia Forster ni za *Thackeray*, *Fielding* na *Charlotte Broute*. Forster anaonyesha kuwa, kwa kutumia wahusika duara, wasanii hudhihirisha hali halisia ya maisha katika riwaya. Aidha msanii hufanya hivi ili kupata dhamira yake.

Forster anaongeza kuwa, msanii bora wa riwaya hutumia wahusika wa aina zote mbili ili kuweza kupata dhamiri yake ya kuzoeza tabia za ugenini na kupatanisha ujamaa wa binadamu na vipengee vingine vya riwaya yake. Hata hivyo, Forster anaona wahusika bapa kuwa muhimu kwa sababu hutambulika kwa urahisi na hubaki akilini mwa msomaji baada ya kusoma riwaya. Kazi ya Forster inaonyesha jinsi msanii hutumia muundo wa uhusika kuendeleza maudhui katika kazi yake. Katika utafiti huu, ilihitajika kurejelea wahusika, hulka na tabia zao na makundi yao mbalimbali ambayo yanakinzana. Hulka na tabia za wahusika ilikuwa sehemu muhimu ya utafiti huu, zilisaidia katika kutathmini ikiwa kuna utatuzi wa matatizo au la. Utafiti huu ulitumia matukio kama deta na matukio, anavyoeleza Todorov(1977) ni mamoja na wahusika. Anasema;

> 'Hakuna mhusika isipokuwa katika tukio, hakuna tukio ambalo linalojisimamia bila mhusika...Mhusika anavyosawiriwa ndicho kisababishi cha tukio na athari zake,yote ni mamoja kama lilivyo tukio lenyewe'(uk67). (Tafsiri yangu)

Dan Izevbaye (1979) anaeleza kuwa mwanariwaya wakati mwingine hutumia mfumo wa kiautografia kwa kuvaa nafsi ya nguli kama mhusika na kuzungumza kwa sauti yake. Mfano mzuri anaoutoa Izevbaye ni Chinua Achebe ambaye anamtumia mhusika Odili katika *A Man of The People* kama mdomo wake na mbinu hii inampa nafasi nzuri ya kutumia ujuzi wake wa kinaya kwa manufaa ya kazi yake zaidi.

Wanariwaya wengine hawajatumia mbinu hii kwa njia ya moja kwa moja. Armah katika *Why are we so Blest* bila ufanisi mkubwa, anatumia shajara, namna ya hadithi katika waraka kwa kuendeleza hadithi ya wahusika watatu ambao walikutana katika Congheria. Izevbaye anaona mbinu hii kama autografia hafifu, kwa sababu wahusika hawapewi uhuru wa kujikuza, mwandishi anawajenga kutegemea mtazamo wake. Aidha anaeleza kuwa kuna hadithi zinazohadithiwa katika nafsi ya tatu, hapa anaelezea Armah kama aliyesimulia hadithi yake kwa kutumia njia hii katika riwaya yake ya pili, *Fragments*. Anaelezea kuwa riwaya hii ni ya kihalisia ambayo iliandikwa kibunifu na inasimuliwa katika nafsi ya tatu hasa katika sehemu ambayo matukio hudhihirika kupitia mtazamo wa nguli. Izevbaye anaona riwaya hii kuwa inayodhihirisha mipaka ya kiautografia katika tungo za riwaya. Utafiti wa aina hii umeshughulikiwa sana katika riwaya. Kazi hii pia iliwarejelea wahusika lakini kwa mtazamo unaojikita katika wanavyokabiliana na kutatua matatizo katika jamii.

Ngara (1982) amechanganua riwaya ya *Arrow of God* (1974) ya Chinua Achebe miongoni mwa riwaya zingine; *The Voice* ya Gabriel Okara, *A Grain of Wheat* ya Ngugi wa Thiong'o, *Season of Anomy* ya Wole Soyinka na *Two Thousand Seasons* ya Ayi Kwei Armah. Katika uchanganuzi wa riwaya ya *Arrow of God*, Ngara anabainisha mseto wa matatizo na migongano mbalimbali. Mathalani, anaeleza kuwa, muktadha wa kijamii na kihistoria ya riwaya hii ni wakati wa majilio ya wazungu na athari zake katika mashariki ya Nigeria. Wakati ambapo wamishonari na wakoloni walitamalaki katika jamii ya 'Waigbo'. Sehemu nyingi za nchi hii zilitawaliwa na wakoloni kutoka Uingereza na ziliathiriwa sana lakini Umuaro bado anaishi kwa kuzingatia utamaduni wake wa kienyeji (Kiafrika). Ngara anaelezea kuwa, wahusika katika riwaya hii wana misingi tofauti ya kiismu na kijamii, anaonyesha kuwa Achebe anatumia migongano

kudhihirisha matokeo ya mwingiliano wa tamaduni na lugha tofauti tofauti. Pijini ni matokeo ya mwingiliano wa lugha tofauti (Kiingereza na lugha za kienyeji). Kazi ya Ngara inakurubiana sana na utafiti huu. Katika riwaya za Burhani, tuliona mgongano wa tamaduni mbili; utamaduni wa kijadi ukishikiliwa hasa na wazee wa ule wa 'kisasa' ukishikiliwa na vijana. Utamaduni wa kisasa kama anavyoelezea Ngara unaendeleza ukoloni mamboleo. Vijana wengi wanahangaishwa na ujana wanapokengeuka kwa kuiga kipofu utamaduni wa kigeni. Katika riwaya za Burhani, kuna wahusika vijana kama vile Ali katika *Mali ya Maskini* na Monika katika *Mwisho wa Kosa* ambao wanahangaishwa na ujana kwa sababu ya kupuuza desturi za kijamii na kukumbatia utamaduni wa kigeni bila ya kuchuja mazuri na mabaya kutoka utamaduni huo.

2.2 Riwaya za Kiswahili

Mlacha (1985) amechunguza wahusika katika riwaya nchini Tanzania kabla na baada ya miaka ya 1970. Anaeleza kuwa, kabla ya miaka ya 1970, wanariwaya walitumia sana wahusika miungu, wanyama na watu dhahania, hali iliyosababishwa na woga wa wasanii kujihusisha na ukweli kwa kuhofia utawala uliokuwepo ungewaandama kwa sababu haukutaka utolewe nakisi. Anatoa mfano wa Shaaban Robert katika *Siku ya Watenzi Wote* na *Adili na Nduguze*. Baada ya mwaka wa 1970, wasanii walitumia wahusika wa kihalisia kama wakulima, vijana na wafanyikazi. Kwa mfano, katika *Nyota ya Rehema* na *Kiu* za M.S Mohamed, *Asali Chungu* ya S.A Mohamed na *Dunia Uwanja wa Fujo* ya Kezilahabi. Katika riwaya hizi, Mlacha anawagawanya wahusika katika makundi matatu makuu: wahusika wakuu, wahusika wasaidizi na wahusika wajenzi. Kazi yake inaonyesha kuwa japo kuna tofauti, aina zote tatu ni muhimu katika kukamilisha kazi ya fasihi. Utafiti huu ni tofauti kwa sababu haukuegemea usawiri wa wahusika bali namna wanavyowezeshwa na mwandishi kutatua matatizo yanayowakabili.

Mlacha (1986) amechunguza muundo wa uhusika na mhusika mkuu katika riwaya ya Kezilahabi; *Rosa Mistika*. Anafafanua uhusiano wa wahusika kwa mhusika mkuu ambaye ni Rosa kwa kuainisha hulka zao tofauti tofauti. Anatumia kigezo karibu sawa na kilichotumiwa na Thurstone (1947) katika *Centroid Factor Method.*

Katika kigezo hiki, ili kuweza kupata sampuli ya vigezo vya kutathmini sawasawa na vya kisemantiki, idadi ya matukio na marudio ya uamili hutumiwa na kupimwa ikiwa kweli inategemeeka, Mlacha anaona njia hii ya utafiti husaidia kutathmini mahusiano baina ya wahusika na kuainisha miundo na mijengo yao tofauti katika riwaya. Katika utafiti huu, nilirejelea pia wahusika lakini sikuchunguza miundo na mijengo yao bali matatizo yanayowakabili na namna wanavyojitahidi kwa kutumia mikakati mbalimbali katika utatuzi wa matatizo hayo.

Senkoro (1987) anajadili kuhusu maendeleo ya riwaya za Kiswahili katika mifumo tofauti ya kijamii. Kwanza anajadili riwaya ambazo zimejitenga na jamii. Zimetungwa tu ili kufurahisha wasomaji. Anatoa mfano wa riwaya za M.S Abdula, E.Ganzel, F.Katalambala na wengineo. Mathalani, katika riwaya za M.S Abdula; *Mzimu wa Watu wa Kale, Kisima cha Giningi, Siri ya Sifuri*, na *Mwana wa Yungi Hulewa,* anaeleza kuwa mwandishi ameshughulikia zaidi suala la kumsisimua msomaji na kumpumbaza kwa visa vya upelelezi, aidha ameshughulikia haki za wanaojiweza tu kama vile wana wa vibwanyenye na vibepari-uchwara waliochuma kwa biashara za ubinafsi na unyonyaji. Katika utafiti huu, tunamwona Burhani kama msanii anayejali jamii kwani anamulika uhalisia na kupendekeza njia za kutatua matatizo yanayoikabili jamii ili kufanya maisha kuwa bora na yenye amani zaidi.

Aidha Senkoro anaongezea kuonyesha kuwa, Abdula si peke yake katika mkumbo huo, zipo kazi zingine ambazo zimejitenga na jamii, katika riwaya za Kezilahabi; *Kichwamaji* na *Dunia Uwanja wa Fujo* kwa mfano, Kezilahabi anayajadili masuala mbalimbali katika jamii na jinsi anavyoyajadili yamejitenga sana na matatizo yaliyomo katika jamii. Mathalani, suala la kuchunguza nini maana ya maisha ni mojawapo ya hayo. Katika kulishughulikia jambo hili, anakatisha tamaa wasomaji kuwa maisha hayana maana wala faida yoyote. Utafiti huu ulionyesha hali tofauti na kinyume kabisa na ya utamaushi anayosawiri Kezilahabi, Burhani anaonyesha kuwa japo kuna matatizo mbalimbali katika jamii, juhudi zinaweza kufanywa ili kuyaondoa na wale walioathiriwa kupewa fursa nyingine kuanza upya maisha iwapo wangekiri makosa yao.

Kwa upande mwingine, Senkoro anachanganua riwaya ambazo zinawatetea wanyonge na kuupinga mfumo wa kibepari. Kwa mfano, riwaya ya M.S Mohamed, *Nyota ya Rehema,* za S.A Mohamed, *Asali Chungu*, *Utengano* na *Dunia Mti Mkavu* na za S A Shafi, *Kasri ya Mwinyi Fuad* na *Kuli*. Anaelezea kuwa kazi zote hizi zilichota maudhui kutoka katika maisha ya harakati za watu wa Unguja walipofanya mapinduzi ya kumtimua Sultani na mamwinyi wengine waliofaidi kutokana na jasho la wanyonge. Utafiti huu unakurubiana na uchanganuzi huo isipokuwa katika riwaya za Burhani, mageuzo hayatokei kupitia mapinduzi makali bali mikakati inayowapa waathiriwa fursa ya kujirudi na kuanza upya maisha yenye amani na salama.

Shija, (1975) ametafitia wahusika wa Shaaban Robert. Anafafanua kuwa, uumbaji wa jamii ya wahusika wa Shabaan Robert unaonyesha vikundi viwili vya wahusika vinavyokinzana. Kimoja kina wahusika wenye sifa na majina yaliyo kinyume katika maana na yale ya kikundi cha pili. Kwa hali ya majina, yaonekana kwamba majina ya wahusika kadhaa yana maana ya wema na yaliyobaki yana asili ya ouvu. Kila mhusika mwenye jina linaloonyesha ouvu naye pia ni mwovu wa sifa, na aliye na jina lenye maana ya wema ni mtenda wema daima.Wahusika wanaodhihirisha wema au uovu kuambatana na majina yao ni kama vile Adili katika *Adili na Nduguze*. Hulka ya Adili ni kinyume kabisa na ya wahusika 'Hasidi' na 'Wivu' ambao pia wamepewa majina kimajazi.

Shija anaelezea kuwa, mtindo huu wa kumpachika jina mhusika ili aonekane mwema au mwovu unaweza kuleta majadiliano makali. Kwa mfano, ni rahisi kusema kwamba wanadamu wana desturi ya kutoa msimbo au jina zuri kufuatana na matendo ya mtu anayehusika, na kwamba katika hadithi ya *Kusadikika* pana Waziri Mkuu wa Kusadikika ambaye matendo yake yalijaa tadi na inda, na kwa hivyo, watu walimpa jina la 'Majivuno'. Mhusika Karama ambaye ni mwema anatenda kulingana na maana ya jina lake. Shaaban anatumia mtindo huu wa majina ili aweze kutoa muhtasari wa wasifu wa wahusika wake. Hii ni njia rahisi ya kumwongoza msomaji kwa kumwonyesha jina ambalo linampa sifa mhusika mahsusi ingawa wakati mwingine ina hatari ya kuuchafua

usanifu. Kwa mfano wakati msomaji anapolazimishwa kuuona ubaya au wema bila ya kupewa muhula wa kutumia uwezo wake wa kuyachambua mema au maovu.

Kazi ya Shija ni tofauti na yetu, hata hivyo wahusika watakuwa muhimu sana katika ukusanyaji wa deta ya utafiti huu. Ilihitajika kurejelea wahusika mbalimbali na namna ambavyo wanakumbwa na matatizo mbalimbali na wanavyokabiliana nayo na juhudi wanazotumia kuyaondoa.

Kamunde (1983) amejadili 'unyonge' wa tabia katika tabaka la juu unavyojitokeza katika *Utengano* (1980), *Asali Chungu* (1978), na *Dunia Mti Mkavu* (1980) Madhumuni ya Kamunde yalikuwa kuwajadili wahusika mbalimbali kwa kadri wanavyobainisha unyonge wao. Maoni ya Kamunde ni kuwa, S.A Mohamed ameeleza kinagaubaga juu ya mifumo itumiwayo kuwadhalilisha wanyonge kama vile siasa, uchumi, na masuala ya jamii. Kazi ya Kamunde ni tofauti na yetu.

Hata hivyo, katika kupambanua aina mbalimbali ya migongano, tuligusia kwa kiasi 'unyonge' wa wahusika mbalimbali kiumri, kiuana, kiuchumi na kadhalika. Kazi yetu hata hivyo, haikutilia mkazo unyonge bali namna unyonge huo unasababisha matatizo na migongano na vile ambavyo Burhani anatumia njia mbalimbali ili kuondoa ama kutatua migongano na matatizo hayo.

Mazrui, (1984) amehakiki riwaya ya *Dunia Mti Mkavu* kwa kutumia nadharia ya Kimarx. Anajadili kuwa, riwaya hii ya S.A Mohamed kufikia wakati huo iliwakilisha kilele cha maendeleo ya riwaya ya Kiswahili katika uchanganuzi wake wa kisiasa na kijamii kuhusu mabadiliko na upembuzi wa jamii za Kiafrika chini ya utawala wa kidhalimu. Kazi ya Mazrui inakurubiana na utafiti huu ila tu umejikita katika usawiri wa matatizo na namna yanavyotatuliwa katika riwaya za Burhani. Tofauti ni kuwa, katika riwaya ya *Dunia Mti Mkavu*, mapinduzi yanayojitokeza yanatekelezwa kwa nguvu na mabavu lakini katika riwaya za Burhani, mabadiliko yanaletwa polepole kupitia juhudi za wanajamii kupatanisha wahusika ama makundi ambayo yanakinzana. Ukuruba wa kazi ya Mazrui na utafiti huu ni kuwa, nilitumia pia nadharia inayohusishwa na Marx; nadharia ya mgongano.

Wamitila (2003) amejadili matatizo na migongano katika riwaya ya *Walenisi* (1995) ya Katama Mkangi. Anaeleza kuwa kuna matatizo kama vile ujinga, magonjwa, dhulma na mgongano wa makundi mbalimbali ya wanajamii. Hali hii inatokana na ubaguzi wa aina mbalimbali, kama vile ubaguzi wa: kiuana - kudhulumiwa kwa mwanamke, kidini, kimadhehebu, ubaguzi wa rangi, kikabila, wasomi/wasiosoma na kiuchumi. Wamitila anaonyesha kuwa, suala linaloibuka ni kuwa, hali hii ni tatizo linalokumba ulimwengu wa sasa. Aina hizi za ubaguzi zimeenea pengi ulimwenguni na mwandishi anatujuza kuwa ikiwa walimwengu wenyewe hawatatambua ukweli huu, basi maisha yao yamo mashakani. Matatizo haya yanayojitokeza katika riwaya ya Mkangi ni ya kilimwengu lakini yaliyojitokeza katika riwaya za Burhani ni mahsusi kwa jamii za Kiafrika. Mkangi pia hatoi suluhisho la moja kwa moja, mandhari anayoyatumia ni ya kidhahania, sio halisia kama ya Burhani. Hata hivyo tuliona ubaguzi wa kiuana, ambapo mwanamke anachukuliwa kama kiumbe duni, hali ambayo si tofauti na ilivyokuwa katika jamii ya riwaya ya *Walenisi* kabla ya mapinduzi kutekelezwa.

Amina Vuzo (1999) amegusia matatizo mbalimbali katika riwaya ya *Siku Njema* iliyoandikwa na Ken Walibora. Anaeleza kuwa riwaya hii imesawiri matatizo kama vile ujambazi, chuki, umalaya, malezi mabaya na kadhalika. Mathalani, katika riwaya, baada ya kifo cha mzee Mwinyi Makame, familia yake iliachwa katika migogoro ambayo hatimaye ilitenganisha familia hiyo kabisa. MwanaSaumu hakupenda ndugu wa mumewe, wakati wote walikuwa katika hali ya mgongano. Zainabu anapokufa mwanawe Msanifu Kombo anaenda kuishi kwa Mwanasaumu. Mwanasaumu anapanga njama kutaka kumuua, kutokana na hiki kitendo, mwanamke huyu anajikuta katika migongano kwa muda mrefu na jamaa zake. Wazazi wa Zawadi hawakutaka binti yao aolewe na Rashid kwa sababu hana asili wala fasili. Jambo hili lilizusha migogoro baina ya wazee na vijana hao. Kazi ya Amina Vuzo ni ya kijuujuu, hazami sana labda kwa sababu hadhira anayoilenga ni wanafunzi wa shule za upili na vyuo vya kati, hata hivyo, kuna ukuruba na kazi hii ambapo Burhani anasawiri matatizo yanayoibuka

kwa sababu ya migongano ya kiaila na unyumba. Kazi hii ilienda hatua nyingine zaidi kuonyesha vile ambavyo mwandishi anatumia mikakati mbalimbali katika juhudi za kutatua matatizo hayo.

Njogu, na Chimerah (1999) wanajadili migongano na vilele vyake katika riwaya ya *Shamba la Wanyama* iliyoandikwa na George Orwel. Kwanza wanaeleza kuwa kuna mgongano baina ya binadamu, wakiongozwa na Mtiki; na wanyama, chini ya uongozi wa Mbalamwezi, Mzushi na Mkimwa. Mgongano huu unafikia kilele cha mapinduzi na Mtiki anatimuliwa shambani. Mgongano wa pili ni baina ya Mzushi na Mkimwa, na unahusu kung'ang'ania madaraka. Kilele cha mgongano huu ni kutimuliwa ama kufukuzwa kwa Mzushi kutoka shambani; nusura auawe. Mgongano wa tatu unasababishwa na wanyama wanaopinga mtindo wa Mkimwa wa utawala unaoneemesha unyanyasaji. Mgongano huu una vilele viwili. Cha kwanza ni cha uasi wa kuku dhidi ya nguruwe wanaowalazimisha kutaga mayai mengi kwa lengo la biashara. Kuku wanakataa na kupaa mitini ambako wanayatagia mayai yao, ambayo yanaanguka na kuvunjika. Kuku wanaadhibiwa kwa kunyimwa chakula. Mgongano huo pia unaingiza wanyama wengine kama vile Mwenge, na Nguruwe wanne waasi. Kilele cha maasi haya ni kuuawa kwa kuku, nguruwe hao wanne, na wanyama wengine wengi waliolazimishwa kukiri kuwa waliasi. Mgogoro mkuu zaidi ni baina ya nguruwe wakisaidiwa na mbwa, na wanyama wengine wote upande mwingine. Mgogoro huu ni mgogoro wa uongozi, na kilele chake ni kugandamizwa kwa wanyama wa tabaka la chini na wale wenye kutawala.

Ugandamizaji huu unakomaa na kuwa udikteta. Matokeo ni kwamba wanyama wengine wote, isipokuwa Mkaidi Mzee Punda, na Mwenge, mbabe wa miguvu, wanaishi kwa uoga shambani humo. Inaweza kusemekana kwamba kukabidhiwa binadamu Mwenge na kuchinjwa kwake ndiyo hatima ya kilele hicho. Kifo cha Mwenge kilifutilia mbali kabisa ukinzani wa aina yoyote dhidi ya utawala dhalimu wa nguruwe. Uchambuzi huu wa Njogu na Chimerah unakurubiana sana na utafiti huu. Tofauti tu ni kuwa, wamechambua wakilenga hadhira ya wanafunzi darasani, kwa hiyo,

kazi yao haijazama sana. Utafiti huu ulizama kwa kiasi na kudhihirisha namna mwandishi anavyotatua matatizo katika jamii katika riwaya zake.

Mwisho katika sehemu hii, ni kuhusu tahakiki ya Njogu (1997) kuhusu riwaya za visiwani Zanzibar. Njogu anaonyesha kuwa kuna maingiliano makubwa baina fasihi na matukio ya kihistoria. Kabla ya mapinduzi ya visiwani Zanzibar, kulikuwa na mivutano mikubwa ya kitabaka baina ya 'walio navyo' na 'wasiokuwa navyo'. Mivutano hii imehifadhiwa katika fasihi ya visiwani. Katika tahakiki yake, Njogu amebainisha namna ya mikinzano ya kijamii, kiuchumi na kisiasa ambayo ilikuwa kichocheo cha mapinduzi. Amechanganua riwaya za visiwani Zanzibar ili kudhihirisha ukweli huu. Mathalani: *Kasri ya Mwinyi Fuad* (1978) ya Shafi Adam Shafi, *Kuli* (1979) *Asali Chungu* (1980) *Dunia Mti Mkavu* (1980 (a)) *Utengano* (1980 (b)) za Said Ahmed Mohammed na *Kiu* (1972) na *Nyota ya Rehema* (1976) za Mohamed Suleiman Mohamed.

Njogu ameshughulikia mada nne kuu: (i) Nadharia, Fasihi na Jamii (ii) Fasihi na Muundo wa Uzalishaji Mali (iii) Mikinzano ya kitabaka na Mapinduzi ya Kijamii na (iv) Usawiri wa Mapinduzi. Kati ya mada hizi nne, inayokurubiana na utafiti wetu ni mada kuhusu mikinzano ya kitabaka na mapinduzi ya kijamii. Njogu anajadili na kuonyesha vile ambavyo mikinzano ya kitabaka ndiyo iliyochochea mapinduzi ya kijamii. Maisha visiwani yalikuwa katika matabaka. Tabaka la juu lilinyanyasa tabaka la chini hadi ikafika kiwango cha kutovumilika tena na maasi yanatokea ambayo yanasababisha kutekelezwa kwa mapinduzi ya kijamii. Njogu ametumia nadharia ya uyakinifu wa kijamii.

Kazi ya Njogu inakurubiana sana na utafiti wetu. Tofauti tu ni kuwa utafiti wetu ulijikita katika riwaya za Burhani, na tofauti na kazi ya Njogu, ulichanganua matatizo yanayoibuka katika mahusiano ya kijamii na namna mwandishi anaweka mikakati mbalimbali ya kutatulia matatizo yanayoibuka. Aidha, badala ya mapinduzi makali yaliyojitokeza katika riwaya za visiwani, tuliona juhudi za wanajamii kuondoa migongano na kutatua matatizo ambayo yangesababisha vita. Ukuruba uliopo ni

kwamba tulitumia pia nadharia inayoegemea mtazamo wa Ki-Marx; nadharia ya mgongano.

2.3 Misingi ya Nadharia

Misingi ya nadharia itajikita katika nadharia ya mgongano kama inavyofafanuliwa na wanasosiolojia. Nadharia hii ina asili yake katika U-Marx, kwa hivyo, nitaelezea kuhusu misingi ya uhakiki wa U-Marx. Wananadharia wa nadharia ya mgongano walitumia mawazo ya Marx na Engels ingawa walitofautiana nao kidogo. Kazi za Marx zinatambuliwa kwa kuweza kutabiri mambo ya usoni na imani ya u wezekano wa jamii shwari, isiyo na migongano. Wachanganuzi wa nadharia ya mgongano walipuuza imani hiyo kama ya kiutopia na kushikilia mtazamo wa Max Weber (1864-1920). Weber alikuwa mfuasi wa Marx ambaye alipanua mawazo ya Marx na kuyafanya yakubilike zaidi na wachanganuzi waliofuata baadaye, hasa wanasosiolojia.

Wanasosiolojia, Stein J.P, Markson W.E, na Hess B.B (1992) katika kitabu chao *Socilogy* wanajadili mikakati ambayo inaweza kutumiwa ili kuondoa migongano na kutatua matatizo yanayokabili jamii. Mathalani, ukaribishaji, mapatano na mashauriano badala ya mapinduzi makali kama vile inavyopendekezwa na Marx.

2.3.1 Nadharia ya Mgongano

Utafiti wetu utajikita katika nadharia ya mgongano. Katika sayansi ya kijamii, nadharia ya mgongano inarejelea mtazamo wa kuchukulia matukio ya kijamii kama matokeo ya migongano kati ya watu binafsi ama makundi ya watu. Nadharia hii imekua na kukuzwa katika viwango vidogo na mapana. Viwango vidogo vinatalii watu binafsi na kutokana na sifa za mtu, hulenga kuzua sifa-bia za kibinadamu.

Wanasayansi wa kijamii huamini chanzo cha tabia za kibinadamu ni kutokana na masharti ya maisha ambayo yana mifumo iliyoratibiwa ya kusababisha ugomvi na kujilinda binafsi. Pia, msukumo wa kibinafsi unaosababishwa na hali za mtu binafsi kama vile matakwa yake, vikwazo na kutupa ama kuhamisha wasiwasi wake wa kindani kwa wengine.

Maandishi ya awali ya wanasaikolojia na wauguzi wa akili kuhusu mgongano wa makundi na vita yalichukulia kuwa tabia za kitaifa ni kujumlishwa kwa tabia za

watu binafsi katika taifa hilo. Mtazamo huo umepingwa ingawa umuhimu wa saikolojia ya kibinafsi umejitokeza upya katika nadharia ya mgongano ya kisasa kwa umbo changamano zaidi. Wanasosiolojia, wanaanthropolojia, wanasayansi wa kisiasa na wanafalsafa wa taratibu na mawasiliano hushikilia mtazamo mpana. Sifa-bia za mgongano si matokeo ya tabia za kibinafsi bali ni tabia ya kijamii inayotokana ama na hisi ya upamoja au ya viongozi kulinda mipaka ya kitaifa au kushinda taifa lingine. Mtazamo huu unafafanua mgongano kama hali ambayo kundi moja bainifu linajihusisha na kupinga kundi lingine bainifu. Hali kadhalika, kushindania mamlaka na rasilmali vilivyo akali, ambapo madhumuni ya wapinzani wao ni kubatilisha, kuumiza ama kuwaondoa wapinzani wao.

Kulingana na wanafalsafa wengine mgongano unaweza kuwa na dhima yakini ya kijamii. Inaweza kuwa njia ya pekee ambayo watu wanaonyanyaswa hutetea haki zao. Wanasayansi wa siasa huchukulia kuwa mgongano au vita ni hali isiyoepukika katika siasa za kimataifa kwa sababu tisho la vurugu ni muhimu ili kujenga udhabiti na kuhifadhi amani, na mgongano au vita huzatiti matakwa yao wanayoshindania. Mwasisi wa nadharia ya mgongano ni mwanafalsafa maarufu Karl Marx (1818-1883). Kazi yake muhumu ya kinadharia ni *Das Kapital* (1867), kazi ambayo ilihusu uchanganuzi wa masuala ya kiuchumi ya mfumo wa ubepari. Baada ya kifo chake, kazi zake ambazo hazikuwa zimechapishwa zilihaririwa na Engels. Pamoja na Engels, walichapisha *The Communist Manifesto* (1848).

Misingi ya Uhakiki wa Ki-Marx

Uhakiki wa Ki-Marx unahusiana na nadharia nyingi. Misingi yake mikuu ni mawazo yanayohusishwa na Karl Marx na Freidrich Engels. Nadharia hii imepitia mabadiliko makubwa na kupata wafuasi wengi. Wahakiki wengi wameitumia kukidhi mahitaji yao, mahsusi ya uhakiki. U-Marx unahusu nyanja mbalimbali kama uchumi, historia, jamii na mapinduzi. Msukumo mkubwa wa nadharia hii unawekewa msingi na kauli aliyoitamka Marx, Wamitila (2000:182) akimzungumzia mwanafalsafa Feurbuch, kuwa 'wanafalsafa wameishia kuufasiri ulimwengu tu (lakini) jambo muhimu ni

kuubadilisha'. U-Marx una sifa ya kijumla inayojitokeza katika mwelekeo wake wa kuligusia kila eneo, na kuwa na la kusema kuhusu takribani kila kitu.

Mawazo ya Marx kuihusu historia na miundo ya kijamii yana nafasi kubwa katika nadharia hii. U-Marx ni falsafa ya kiyakinifu hasa kwa kuwa pana msisitizo mkubwa kwenye msingi wa hali za kiyakinifu za maisha ya binadamu. Marx hauegemezi mfumo wake kwenye dhana dhahania kama urembo, ukweli au ndoto bali uhalisia unaoonekana. Mawazo ya Marx kuhusu uyakinifu yametolewa nakisi na kutajwa kama ya kindoto. Kwa kweli, hali ya jamii kuwa katika hali ya pasi na mgongano aliyotabiri Marx haijapatikana popote ulimwenguni na huenda isipatikane kamwe katika miaka inayokuja. Hata hivyo, mawazo yake kuhusu kuwepo kwa migongano ya kitabaka katika jamii yana mashiko na ndiyo msingi wa nadharia ya mgongano. Uyakinifu aliyourejelea Marx unadhihirika katika jamii na umeweza kusawiriwa katika kazi nyingi za kisanaa.

Migongano ya kitabaka katika jamii nyingi imesababisha kutekelezwa kwa mapinduzi kwa njia ya upanga na tabaka linalonyanyasa mengine kung'olewa mamlakani. Hata hivyo, mageuzo yametokea pia kupitia mikakati ya mashauriano na mapatano, njia hii ndio inayopendekezwa na wanasosiolojia katika nadharia ya mgongano. Burhani kama mwandishi ameepukana na matumizi ya njia ya upanga kuleta mageuzo katika jamii na kupendekeza mikakati ya mashauriano na mapatano. Kwa hivyo, yamkini uyakinifu aliourejelea Marx wa kuwepo kwa mikinzano na migongano ya kitabaka utaendelea kudhihirika katika nyanja tafauti za maisha lakini kiwango cha jamii kuwa na usawa pasi na mgongano wowote ni kitu ambacho kitabakia tu ndotoni. Baadhi ya misingi ya nadharia hii ni kama ifuatavyo:

Kwanza, historia ya maisha ya binadamu inaweza kuelezeka katika misingi yakinifu ya kiuchumi; njia za uzalishaji mali pamoja na miundo ya kiuchumi inayoathiriwa sio uzalishaji wa mali hiyo tu bali na usambazaji wake.

Suala hili la uzalishaji na usambazaji wa mali linaunda kile ambacho hujulikana kama 'msingi'. Kwenye msingi huo ndiko kunakotegemezwa muundo wa juu au

'kikorombwezo'. Kikorombwezo ndicho kinachohusisha maadili, itikadi, dini, utamaduni, na kadhalika.

Pili, wahakiki wa Ki-Marx wanaamini kuwa daima historia ya binadamu itadhihirisha au kuakisi harakati zinazoendelea katika matabaka ya kiuchumi-jamii. Marx na Engels walidai kuwa kitu cha msingi katika maisha ya binadamu ni kula na kunywa, kupata malazi na mavazi na mahitaji mengine ya kimsingi. Kwa hivyo, tendo la kwanza kihistoria ni kutafuta njia kuyakidhi mahitaji haya ya kimsingi. Ili kufanikiwa katika lengo hilo, binadamu hulazimika kujiunga pamoja au kuunda umoja ili kuimarisha ubora na wepesi wa kuizalisha mali ya kukidhi mahitaji hayo. Muungano huo huwa na ugawaji wa majukumu au kazi ambayo ndio msingi wa kuundwa kwa matabaka katika jamii. Aidha, huzuka mfumo wa ubepari ambao kwao, mali inamilikiwa na idadi ndogo ya watu.

Watu hao wachache wanaipata mali yao kutokana na unyonyaji wa umma na hasa wafanyikazi. Kadiri mfumo wa ubepari unavyoendelea kukua ndivyo tofauti kati ya matabaka zinaimarika kwa sababu kuna watu wanaofaidika kwa njia zisizo za haki. Kufaidika huko kwa njia zisizo za haki pamoja na mbegu za kujiangamiza zilizomo kwenye mfumo wenyewe. Marx aliamini kuwa haya yanayotokana na mfanyiko wa kiasilia wa kihistoria; historia huendelea kutokana na mfululizo- safu wa mkinzano wa mawazo. Matokeo ya mkinzano huo ni kuzuka kwa hatua nyingine mpya ya kihistoria. Mathalani, kuanzia enzi ya ujima, kupitia umwinyi, ubepari, ujamaa ambao si unakurubiana na ujima, ukomunisti na hatimaye utopia, hali ambayo watu wote watakuwa sawa bila ya mikinzano na migongano ya aina yoyote. Hali hii ya kiutopia ni ya kindoto na huenda isipatikane ama kufikiwa na jamii.

Tatu, matamanio na matakwa ya matabaka yaliyopo katika jamii na hasa tabaka lenye nguvu yanaakisiwa katika itikadi iliyopo katika jamii, jinsi na miundo ya mawazo ambayo aghalabu huwa imeshika kwa nguvu na huwapo kila mahala kiasi cha kuwa wanajamii wasiitambue kwa haraka. Hali hii huwa imesitiriwa katika 'ung'amuzibwete' wa jamii. Hali ambayo huweka jamii katika migongano kwa sababu ya kukinzana kwa matamanio na matakwa ya matabaka mbalimbali. Fasihi inayojitokeza inaweza

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY

kuyaakisi na kuyadhihirisha mahusiano hayo ya matabaka na matumizi ya nguvu kwa kila tabaka likijitafutia nafuu na kukidhiwa kwa matamanio na matakwa yake katika jamii.

Nne, kuhusiana na mawazoya Marx, wahakiki wanaamini kuwa ubepari kama njia ya uzalishaji mali utaharibiwa na kuvunjiliwa mbali kutokana na juhudi za wafanyikazi au ubebari utaishia kujiangamiza wenyewe kutokana na mbegu za maangamizo unazozisheheni.

Tano, njia ya kumsaidia, na labda hata kuharakisha kuangamizwa kwa mfumo wa kibepari ni kudadisi, kukosoa, kushutumu, kulaumu na kufichua batili iliyopo katika itikadi ya kibwanyenye inayouimarisha ubepari. Wakati mwingi, hili limekuwa jukumu muhimu la waandishi wa kifasihi. Waandishi wengi wa fasihi wanaoegemea mwelekeo huu wamefichua ubaya na uovu wa mfumo huo kama tunavyoona katika riwaya ya *Asali Chungu* ya S.A Mohamed na *Shetani Msalabani* ya Ngugi wa Thiong'o.

2.3.2 Migongano Mbalimbali

Katika jumuiya ya binadamu, migongano huibuka katika nyanja tofauti za maisha. Wananadharia wa mgongano wamefafanua migongano ya namna mbalimbali. Mathalani, Collins (1975), Friedman (1977), na Edwards (1978) waliochangia kuhusu utawala wa mabwana, Malotch (1976) na Whitt (1982) - miji kama uwanja wa migongano, Bonga (1936), Sutherland (1949) na Coleman (1985) – mkengeuko, Engels (1884/1962), Hartman (1981) na Safilios (1976) – mgongano wa kiaila na kijinsia miongoni mwa wengine wengi walioshughulika maswala mengine mbalimbali.

2.3.2.1 Utawala wa Mabwana

Wananadharia wa mgongano wanasema matakwa ya kiutawala hukidhi matakwa ya wale wenye mamlaka. Kwa hivyo, madaraka siyo mfumo shwari bali uwanja wa mgongano wa matakwa ya matabaka ambapo masuala ya kijamii na mahusiano ya kimamlaka yanayojitokeza katika jamii. (Collins 1975). Wanasayansi wa kijamii wanaofuata falsafa za Karl Marx wanaona utawala wa mabwana kama dhihirisho la kuwepo kwa ubepari na kama chombo cha tabaka moja kukalia mengine.

Wanachanganua madaraka katika muktadha wa tofauti zilizomo katika jamii na huona kwamba ugawanaji wa mamlaka na utoaji wa zawadi kati yao humulika muundo wa matabaka ya kijamii kwa mapana. Katika *Das Kapital (1867/1967),* Marx alidai kuwa kiwanda cha kisasa ni utawala wa kiimla unaosababishwa na mashindano katika soko. Hayo mashirika huwalazimisha mabepari kutafuta watu wa kazi ambao hawana uwezo na wenye gharama ya chini. Ili kutimiza matakwa haya, mabepari huchagua mikakati ya kiteknolojia ili kuwafanya wafanyi kazi wawe wa kubadilishana nafasi na pia wepesi wa kuchezewa na kudhibitiwa. Aidha, Marx aliona kiwanda kama kalibu cha mapinduzi: utawala wa tabaka la wafanyikazi kwa mtaji waweza kutokea kinyume 'uasi wa tabaka la wafanyikazi'. Mitaala ya hivi karibuni ya wanasayansi wa kijamii wa 'Ki-Marx' inaonyesha kuwa utawala wa mabwana ulizuka kutokana na uhitaji wa mabepari kuweka nidhamu ya kazi na mawazo dhahania ya ustadi wa urazini. Hali hii hatimaye inawaendea kinyume mabepari hawa.

Ukweli wa madai haya unadhihirika katika baadhi ya riwaya za Kiswahili. Katika riwaya ya *Asali Chungu* na *Dunia Mti Mkavu* za S. A Mohamed kwa mfano, tabaka la juu linawanyonya wale wa tabaka la chini. Tabaka la kina Zuberi linakandamiza tabaka la walio wengi kwa njia mbalimbali hadi maasi yanazuka na mapinduzi yanatekelezwa. Hali kama hiyo inatokea kwa tabaka la Hamond na Fuad katika *Dunia Mti Mkavu*, ambao vifo vyao ni ishara ya kushindwa kwa umwinyi. Hali ya utabaka pia upo katika riwaya za Burhani, ila tu uasi unaotokea hauishii mapinduzi makali hatimaye.

2.3.2.2 Miji Kama Uwanja wa Mgongano

Mgongano ni sifa moja ya kimsingi ya miji. Miji inaonekana kama uwanja wa mashindano. Wananadharia wa nadharia hii wanasema maisha ya mijini hutegemea eneo muhimu la miundo ya kijamii, mamlaka na matabaka. Ardhi, jambo la kimsingi la pahali, ni bidhaa ya soko inayotoa mali na mamlaka. Wale walio katika nafasi ya juu ya muundo wa mamlaka hufanya maamuzi kuhusu matumizi ya ardhi, makadirio ya umma na maisha ya kijamii ya mijini. Washindi kila mara ni wenye mamlaka na pesa, na

washinde ni maskini na makundi na makundi madogo. Kijumla kiundo cha kimazingira na sifa za kijamii ni dhirihisho na matokeo ya mgongano (Malotch, 1976; Whitt, 1982).

Mwanasosiolojia Malotch (1973,1976) anafafanua wazo hili zaidi kwa kusema kuwa, tuna nguvu na matakwa katika vipande vyetu vya ardhi. Thamani ikipanda, vivyo hivyo, mali yetu inaongezeka. Kila kipashio cha jamii hujaribu, kwa gharama ya wengine kuongeza uwezo wa matumizi ya ardhi yake. Wenye maduka katika kila pembe hushindana kuamua kituo cha basi kitakuwa mbele ya duka hili au lingine, wenye mahoteli hushindania kuwa na chumba cha mikutano karibu nao. Pahali tofauti hupigania kuwa na barabara kuu, bustani, uwanja wa ndege, vyuo na kadhalika. Jiji kwa hivyo, ni mseto wa vikundi vinavyovutana kwa sababu ya matakwa yao mbalimbali.

Wakereketwa wa falsafa za Marx wanasema haja ya kupata faida ndicho kiini cha maovu ya sasa ya maisha ya mijini. Bepari atakaa pahali hadi amalize uwezo wa kujipa faida kisha ahamie kwingine kutafuta faida nyingine, wanaongeza kuwa miji ya kisasa ilichipuka na kupitia mabadiliko ili kukidhi mahitaji ya ubepari (Harvey, 1985). Hata hivyo, nadharia hii haitoi sababu tosha kwa nini miji ya kijamaa/kisosiolisti ya kisasa inafanana na miji ya kisasa ya kibepari. (Castells 1977; Szelyni, 1978). Pia inatoa kidokezo finyu kuhusu kukua na kubadilika kwa miji.Tunaona kwa kiasi ukweli wa madai haya katika riwaya za Burhani ,hasa *Mali ya Maskini* ambapo tunaona wenye biashara ndogo wakifilisika na kuwa maskini kwa sababu ya mashindano na wenye biashara kubwa kubwa.

2.3.2.3 Mkengeuko na Mpisho

Wananadharia wa mpisho wa utamaduni wanasisitiza kuwa watu wa tamaduni tofauti huwa na tabia tofauti kwa sababu wamejamiishwa katika mila zenye kaida na maadili za kipekee. Kutokana na wazo hili, wananadharia wa mgongano wanakubali kuwa makundi huwa na tofauti za kaida na maadili lakini tatizo ni wakati ambapo kundi moja linaweka kaida na maadili yake katika jamii na kutaka yakolee. Hapo ndipo mgongano unatokea. Matakwa ya makundi haya yanagongana kwa sababu ya tofauti zingine kama vile kitabaka, kiuana, kiumri, kirangi, kikabila na kadhalika, swali la kimsingi ni kundi gani linafaidi zaidi kutokana na mambo ya jamii.

Kwa mujibu wa wakereketwa wa 'U-Marx', tabaka la kibepari ambalo linatawala huwanyanyasa na kuwaibia raia walakini hukwepa adhabu kwa maovu yake. Waathiriwa wa udhalimu wa kibepari husukumwa kutenda vitendo ambavyo tabaka linalotawala huviona kama ni uvunjaji wa sheria (Bonger 1936). Aina nyingine za mkengeuko ni kama vile ulevi, kutumia dawa ya kulevya, ugomvi wa kifamilia, uasherati; umalaya na kadhalika vyote vikiwa ni matokeo ya muundo wa kijamii uliojengeka kwa tamaa ya kutafuta faida na kutiishwa kwa maskini, weusi, wanawake na makundi mengine madogo madogo. Matatizo ya kiakili na kijamii hutokea kwa sababu watu wametengana na kuvunja urafiki wao. Kufarikisha uhusiano mzuri hutokea wakati ambapo watu wanatengwa kutoka kwa nyenzo zao za kujipatia riziki. Katika riwaya za Burhani, tunaona mkengeuko wa vijana ambao wanakaidi mila na desturi za jamii yao wakitaka kujitafutia uhuru. Vijana hawa wanaishia kujiingiza katika ulevi, matumizi ya madawa ya kulevya, uasherati na kadhalika

Mtazamo wa mgongano umewafanya wanasayansi wa jamii kuchunguza jinsi ambavyo kuunda na kutekelezwa sheria kunadhibitiwa na matakwa ya wenye mamlaka. Wanasosiolojia wengi wametambua kuwa uvunjaji sheria hufafanuliwa kwa msingi ya maovu dhidi ya mali, kama vile wizi na ubadhirifu wa mali ilhali ufisadi unaofanywa na makampuni na wenye mamlaka hupuuzwa. (Sutherland, 1949; Coleman, 1985). Aidha, adhabu kwa maovu dhidi ya mali ni kufungwa jela kwa wachochole ilhali ufisadi wa mashirika na makampuni huadibiwa kwa kupigwa faini tu. Ukweli wa madai haya unadhihirika katika riwaya ya *Dunia Mti Mkavu*, ambapo mahakama inatumiwa kwa manufaa ya wale wanaomiliki nyenzo za uzalishaji mali. Watetezi wa haki za wanyonge, kama vile mzee Gae wanafungwa kwa mujibu wa sheria zilizotungwa kulinda maslahi ya mamwinyi na mabepari.

2.3.2.4 Elimu

Taasisi za kielimu huvyaza na kuhalalisha muundo wa jamii uliopo. Kwa kufanya hivyo, huwatumikia watu wachache kwa gharama ya wengine (Collins, 1977, 1979). Katika *In Schooling and Capitalist America,* Samuel Bowles and Herbert Gintis wanakiri kuwa mahusiano ya kijamii ya kazi hudhihirishwa katika mahusiano ya

kijamii ya shule. Wanasema shule humulika pahali pa kazi na katika maisha ya kila siku huandaa na kujamiisha watoto waafiki nafasi zao za utu uzima katika soko la kazi. Muundo wa shule huvyaza mfumo wa kiimla kwa kutuza upole, ukubalifu, na heshima; na mtihani unaotumiwa kutathmini wanafunzi ni sambamba na mfumo wa ujuzi wa kuwatia motisha wafanyikazi. Shule, kwa hivyo, hujamiisha kundi la wafanyikazi linaloafikiana na mfumo wa kibepari.

Shule ni nyenzo za kuyajamiisha makundi madogo ya wasiobahatika waingie katika tamaduni ambazo zinatawala ama zenye uwezo. Mwanasosiolojia Collins (1979) anasema kuwa, mfumo wa elimu hutumikia matakwa ya makundi yanayotawala kwa kufanikisha uwezo wa makundi ya kikabila. Elimu ya lazima hufifisha utofauti na itikadi za makabila mbalimbali na kuwashirikisha wanyonge maadili na mienendo ya kimaisha ya wale wenye nguvu. Shule kwa hivyo ni kama vyombo vya kudhibiti. Ukweli wa madai haya unadhihirika katika maisha ya Asumini katika *Tata za Asumini,* riwaya ya S.A.Mohamed, wakati anapojiunga na chuo kikuu, anastaajabishwa na maisha mapya na tofauti ambayo yanamshinda kuyaishi. Wanafunzi wenzake kama Miriam na Sewa wamejamiishwa na kuafiki mfumo wa shule ambao ni wa kimagharibi. Asumini anaporudi kwao, anashindwa kuafiki maisha yanayomngojea, hali ambayo hatimaye inakuja kumwangamiza baada ya kuwa kichaa.

2.3.2.5 Aila (Familia)

Wananadharia wa mgongano huona aila kama mpangilio wa kijamii unaofaidi watu fulani. Friendrich Engels (1884.1902) ambaye ni mfuasi wa Marx aliona familia kama mfano wa matabaka ya kijamii kukiwa na tabaka moja la wanaume linalolinyanyasa tabaka la wanawake. Alisema kuwa ndoa ni mfumo wa kwanza wa ushindani ambapo wenye uwezo huwanyanyasa wanyonge (wanawake) kichocheo cha utawala wa kiuana ni kuwanyonya wanawake kikazi.

Hartman (1981) anasema familia imechukuliwa kama 'nguvu za kijamii' sambamba na mageuzo ya kiuchumi, matabaka na kadhalika. Mtazamo wa mgongano wa kiaila umejitokeza katika viwango tofauti tofauti. Namna moja ya utafiti unamulika mahusiano ya uwezo katika familia, hasa katika kufanya maamuzi. Utafiti unaonyesha

kuwa, kijumla, washiriki wa familia wenye mali zaidi huwa na mamlaka katika ndoa. Safilios (1976) anapambanua kuwa 'upendo' ni sehemu ya picha ya mamlaka katika ndoa.

Utafiti wake ulionyesha kuwa mwenzi wa ndoa mwenye 'upendo' mkubwa ana mamlaka kidogo kwani yeye ni wa kumtegemea mwenzake zaidi – na wenzi ambao wanajiona kama wanapendana sawasawa yamkini hugawana mamlaka. Kulingana na Safilios, mwenzi anayeelekea kupenda zaidi ni mke. Ndoa inakuwa kama biashara ambapo mke hutoa 'upendo' ili apate fadhila kutokana na mali nyingi alizo nazo mume. Familia inachukuliwa kama ulimwengu mdogo wa mgongano katika jamii nzima.

Fasiri ya kisasa ya mtazamo wa mgongano wa kiaila ni ile ya Hartman (op cit) ambayo inafafanua kuwa, familia inaeleweka vizuri zaidi si kwa misingi ya mahusiano ya kihisi au kiukoo bali kama uwanja wa mashindano. Ni pahali ambapo uzalishaji kiuchumi na ugawanaji hutokea na matakwa ya kila mshiriki huwa katika hali ya mgongano na matakwa ya washiriki wengine na yale ya kijamii kijumla. Migongano hii huhusisha mivutano kuhusu nani anapata pesa zaidi, nani anafanya kazi za nyumba, kodi kiasi gani analipa serikali na kadhalika. Hartman (1981) anapambanua kuwa, kukua kwa mfumo mkuu wa kibepari kumeweka rasilmali mikononi mwa mabepari na wanaume. Mgongano huu wa kifamilia unadhihirika vizuri sana katika familia ya Maksuud katika riwaya ya *Utengano*. Tunaona jinsi ambavyo Maksuud ananyanyasa mkewe kama kijakazi huku yeye akijistarehesha anavyotaka na wanawake wengine. Hali hii ni tofauti katika *Asali Chungu* ambapo tunaona familia ambayo kila mmoja; mume na mke ana mali yake, Zuberi kwa upande wake na Amina kwa upande mwingine na ikawa wote wanamtumia Binti Dandi kama mshauri wa kuendeleza starehe na anasa zao. Katika riwaya za Burhani, hali hii inajitokeza ambapo tunamwona Hasani akimdhibiti na kumnyanyasa mkewe Muna katika *Mwisho wa Kosa* na Ali akimtesa mkewe Alama katika *Mali ya Maskini*.

2.3.2.6 Uana

Wananadharia wa mgongano wanasema kuwa, ugawaji kazi kiuana ni chombo cha kijamii kilochoundwa na wanaume ili kijihakikishia nafuu, hadhi na mamlaka

katika mahusiano yao na wanawake. Kwa kuwazuilia wanawake nyumbani, wanawanyima wanawake nguvu ya kufaulu katika ulimwengu mpana. Collins (1975); Vogel(1983). Utofauti wa kiuana umefasiriwa kwa namna tofauti tofauti. Baadhi wanafafanua kuwa kichocheo cha utofauti wa kiuana kinatokana na unyanyasaji wa kiuchumi wa wanawake. Wengine wanasema kinatokana na haja ya wanaume kukidhi ashiki zao za kimwili; wanaume hujitwalia na kulinda haki zao za kupata huduma zao za ngono wanavyotaka vile ambavyo matabaka ya juu hufanya kwa masuala ya kiuchumi.

Toka jadi, ruwaza za utofauti wa kiuana zimeendelezwa kwa kumpa mwanamume nafasi ya mahitaji ya familia na mwanamke nafasi ya kuzaa watoto. Ugawanaji wa kazi umemfunga mwanamke katika jukumu hilo la kuzaa watoto. Kazi za nje hutuzwa kwa mshahara, hadhi na uwezo ilhali za nyumbani zinadunishwa. Mwanamke katika jamii nyingi, amechukuliwa kama mali ya mwanamume. Mwanamke amechukuliwa kama kijakazi nyumbani na chombo cha ngono ili apate usaidizi wa kifedha. Katika mpangilio huo, kuna unafiki mkubwa kwani mwanamume ana uhuru mkubwa wa kingono na kutembea, uhuru ambao mwanamke haupati. Hata hivyo, mfumo wa kisasa wa kiuchumi ambao unamruhusu mwanamke kufanya kazi na kupata ujira umemnasua mwanamke kutoka dhulma za wanaume. Mabadiliko haya yamedhoofisha kaida na maadili ya kijamii ambayo yalimpa mwanamume uhuru mkubwa (Ross 1987). Hali hii imekuwa ni kichocheo cha mgongano wa kiuana. Mtazamo huu si tofauti na tulioona hapo juu kuhusu familia. Tofauti tu ni kuwa, sasa unarejelea wanawake kama vifaa. Tunaona vile ambavyo wanawake wanatumiwa kama vifaa katika riwaya za Kiswahili. Kunao wanaoingilia ukahaba ili kujikimu kama vile Semeni na Maimuna, aidha, Zuberi anawatumia mabinti wa watu kuzimia ashiki zake za kimwili. Anamnajisi Semeni na anamwagiza mzee Omari amletee binti wake. Haya yanajitokeza katika *Utengano* na *Asali Chungu.* Katika riwaya za Burhani, tunaona Ali katika *Mali ya Maskini* akiendelea kuwa na uhusiano na Keti baada ya kuozwa mke, Alama.

2.3.2.7 Dini

Dini inachukuliwa kuwa chombo muhimu cha muungano wa kijamii na umoja lakini wananadharia wa mgongano wanaelezea dini kama chombo cha kuwatumikia wenye mamlaka ambao wanaitumia kudhibiti mivutano inayovyazwa na utofauti wa kijamii na udhalimu. Mengi yanajadiliwa na wanafalsafa kuhusu dini. Mathalani, Karl Marx (1884); Yinger (1957); Glock, Ringer na Babbie (1967). Lakini nitaelezea machache tu kwa sababu suala la dini si dhahiri sana katika riwaya za Burhani.

Dini imeonekana kama chombo cha kuhalalisha mabadiliko yanayopendelea watu wenye mamlaka na mali. Kwa mfano ukoloni na ubaguzi wa rangi umeungwa mkono na kichocheo cha kidini. Kwa hivyo, dini yaweza kuwa ni chombo chenye nguvu kinachotumikia mfumo unaotawala. Inalinda matakwa ya wenye mamlaka kama vile ardhi, mali, uwezo na kadhalika. Mfano mzuri ni Maksuud katika *Utengano* ambaye anatumia dini kuficha maovu yake, hata anajitia usheikh ili aonekane mtu wa dini. Hata hivyo, za mwizi ni arobaini, ujanja wa Maksuud unakuja kujulikana kwa aila yake.

2.3.2.8 Usawa wa Kijamii

Nadharia ya mgongano wa usawa wa kijamii hushikilia kuwa mfumo wa matabaka upo kwa sababu unawafaidi watu fulani wa makundi yenye uwezo wa kuyadhibiti na kunyanyasa makundi mengine. Matakwa yanayowagawanya watu katika matabaka yanatiliwa maanani. Jamii inachukuliwa kama uwanja ambapo watu wanapigania nafuu, hadhi na mamlaka. Mchango mkubwa unatokana na mawazo ya Karl Marx. Marx aliamini mitazamo ya kihistoria ni muhimu katika kufahamu jamii yoyote. Ni muhimu kuzingatia vile ambavyo jamii ilikua kupitia hatua mbalimbali. Hali ya sasa ya kiteknolojia na mfumo wa uzalishi mali ni vigezo vya kimsingi vinavyoamua mageuzo katika jamii. Katika kila hatua ya kihistoria, vigezo hivyo vinaamua ni kundi gani litatawala jamii na makundi gani yatatawaliwa. Katika mfumo wa kifalahi, mabwenyenye walidhibiti uchumi na kutawala mafalahi. Katika mfumo wa kibepari, nafasi ya bwenyenye ilichukuliwa na bepari wa kisasa na nafasi ya falahi na mfanyikazi anayenyanyaswa.

Marx alionelea kuwa, msukumo wa bepari kupata chumo la ziada ndio msingi wa mvutano wa matabaka ya kisasa – mgongano mkubwa wa dhamira kati ya wafanyikazi na mabepari. Mabepari hawatengenezi chumo la ziada bali huvyaza kwa kunyonya nguvu za wafanyikazi. Marx aliwasawiri mabepari kama wezi wa matunda ya nguvu za wafanyikazi. Ulimbikizaji wa mtaji (mali) hutokana na chumo la ziada na ndiyo njia ya ukuzaji wa ubepari wa kisasa. Marx aliamini mivutano ya kitabaka ingesuluhishwa wakati ambapo tabaka la wafanyikazi lingepindua tabaka la mabepari na kuanzisha mfumo mpya wa kijamii. Katika utafiti huu, hali hii haidhihiriki moja kwa moja kwa sababu mapinduzi hayatekelezwi. Hata hivyo, katika riwaya za visiwani kama vile za S.A Mohamed, ukweli wa madai haya unaonekana ambapo, tabaka la juu (la Maksuud na Zuberi) katika *Utengano* na *Asali Chungu,* linawakandamiza watu wanyonge na wanawake. Hatimaye mapinduzi yanazuka na tabaka hilo la juu kupinduliwa.

2.3.3 Mikakati ya Kuondoa Mgongano

Migongano huibuka kutokana na matatizo yanayoikumba jamii. Migongano hiyo hujua na kufikia kilele na kusababisha uhitaji wa kuiondoa ili kutatua matatizo hayo. Kwa hivyo, jamii imebuni njia za kuondoa hali hiyo ya mgongano ndiposa kupunguza ama kutatua matatizo yanayoikabili. Kuna mikakati mitatu ya kuondoa mgongano ambayo imependekezwa na wanasosiolojia wanaozingatia nadharia ya mgongano. Mikakati hii ni ya kutafuta suluhisho la kudumu. Kila upande katika mgongano huchukulia kuwa matakwa yake ni sahihi. Hisi ya usahihi hufanya watu kuingilia tabia ambayo haikubaliki katika hali zingine. Kwa sababu mgongano wa kijamii na wa kibinafsi waweza kuvuruga misingi ya kijamii, kuna haja ya kutafuta suluhisho kwa matatizo yanayokabili jamii. Kulingana na Stein et al (1992:87) mikakati hiyo ni : ukaribishaji, upatanisho na kuondoa uhasama kiitikadi.

(i) Ukaribishaji

Ukaribishaji hutokea ambapo kundi linalokaidi linavutwa na kumezwa na kundi lenye uwezo. Kutokana na mfanyiko huu, matakwa ya kundi linalokaidi yanafifishwa hivi kwamba hakutakuwa na haja ya mgongano tena. Mkakati huu

unatumika sanasana wakati ambapo vijana waliokaidi mila na desturi za jamii wanarudiwa na wazee wao.

(ii) Upatanisho

Upatanisho ni hali ambayo kwayo, mtu wa tatu hutumiwa kusuluhisha mambo. Mathalani katika migongano ya usimamizi wa ajira katika kundi dogo na mapatano katika kadhia za talaka. Mkakati huu unatumika aghalabu wakati mtu ama kundi fulani limekosewa na mta au kundi lingine. Mtu wa tatu hutumiwa ili kupatanisha makundi haya. Mtu au kundi linalohisi kuwa limekosewa linapatanishwa na lile lenye kukosea.

(iii) Kuondoa uhasama kiitikadi

Hii ni njia inayotumiwa na baadhi za jamii na makundi kudhibiti mgongano. Wanaanthropolojia wameripoti kutumiwa kwa njia hii miongoni mwa makundi yaliyomo katika vita ama kati ya jamii jirani (Dirks 1988). Migongano ya kimaeneo nchini Marekani aghalabu huhamishwa kwa timu za riadha. Kuondolewa kwa uhasama kiitikadi hutokea wakati ambapo uhasama hujitokeza katika hali zilizodhibitiwa. Mkakati huu haujitokezi moja kwa moja katika riwaya za Burhani. Hata hivyo, kuna ukuruba na mikakati kama vile mashauriano yanayofanywa ili kutafuta suluhisho kwa watu ama makundi yanayokinzana.

Katika utafiti huu, tulionyesha juhudi za jamii katika kutafuta suluhisho ili kuondoa matatizo yanayoambatana na migongano inayojitokeza. Kila penye matatizo hutokea migongano. Migongano inapofikia kilele, wanajamii hutafuta mikakati ya kuiondoa. Mikakati iliyopendekezwa na Stein et al kama ilivyojadiliwa hapo juu ilinisaidia sana katika utafiti huu kwani ilikuwa kama msingi wa kutambua na kuainisha mikakati aliyotumia Burhani katika riwaya zake.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.0 Utangulizi

Sehemu hii itajadili mbinu zilizotumiwa katika utafiti huu. Utafiti huu ulitumia utaratibu wa upekuzi wa yaliyomo katika vitabu katika ukusanyaji wa deta. Vitabu vilivyotumika ni riwaya za Burhani, *Mali ya Maskini* na *Mwisho wa Kosa.* Katika uchanganuzi wa deta, niliutimia mbinu ya kithamano.

3.1 Ukusanyaji Deta

Katika ukusanyaji wa deta, utafiti ulitumia utaratibu wa upekuzi wa yaliyomo katika vitabu. Mugenda. na Mugenda (1999:174) wanaelezea dhamira kuu ya mbinu ya upekuzi kuwa ni kutalii maandiko kama vile vitabu, magazeti, mapicha na kadhalika ili kuyakinisha hoja zinazoelezea tukio fulani mahsusi.

Katika kutumia utaratibu wa upekuzi wa yaliyomo kukusanya deta ya utafiti, njia zilizozingatiwa ni kama zifuatazo:

(i) Kutafuta vitabu ambavyo vingetumiwa; riwaya za Burhani-*Mali ya Maskini* na *Mwisho wa Kosa*, kisha kuvidurusu kwa kina.

(ii) Kudondoa matukio yote ambayo yanadhihirisha kuwepo kwa matatizo na yale yanayoonyesha juhudi za wahusika katika kutatua na kuondoa matatizo hayo.

(iii) Kupanga deta za utafiti na kuweka katika makundi kulingana na aina ya tatizo na mikakati iliyotumika katika utatuzi wa matatizo hayo ili kazi ya utafiti iwe rahisi wakati wa uchanganuzi wa deta.

Katika kuzingatia hatua hizo tatu katika ukusanyaji wa deta, niliongozwa na misingi ya nadharia ya mgongano. Katika nadharia hii, aina mbalimbali ya migongano katika mahusiano ya kijamii imefafanuliwa katika 2.3.2 na mikakati inayotumiwa katika kuondoa migongano hiyo na kutatulia matatizo hayo, kama ilivyofafanuliwa katika 2.3.3. Deta ya utafiti ni matukio yanayodhihirisha matatizo na namna mwandishi

anatumia mikakati mbalimbali katika utatuzi wa matatizo hayo. Nadharia ya mgongano ina usuli wake katika U-Marx.

Baada ya Max Weber kupanua mawazo ya Karl Marx na kuyafanya yakubalike na kuweza kutumika katika nyanja mbalimbali, wanafalsafa mbalimbali wamebainisha aina nyingi za migongano ambayo inaibushwa matatizo katika jamii na kupendekeza mikakati ya kutatulia matatizo hayo.

Nadharia hii ilisaidia katika kutambua deta za utafiti. Deta ya nadharia tete ya kwanza ikiwa ni matatizo mbalimbali ambayo yamejengeka katika migongano ya aina tofauti na ya pili ikiwa mikakati iliyotumiwa katika utatuzi wa matatizo yaliyomulikwa. Pili, nadharia ilisaidia katika kuainisha matatizo mbalimbali kwa mujibu wa aina ya tatizo.

Utaratibu huu wa upekuzi wa yaliyomo ulifaa utafiti wetu kwa sababu mbili muhimu. Kwanza, utaratibu huu unazingatia iktisadi kwa kuhitaji gharama ya chini kifedha na wakati unaohitajika pia ni mfupi. Hali hii inatokea kwa sababu ukusanyaji wa deta haushughulishi sana kama ilivyo katika taratibu zingine. Utafiti wetu haukuwa na ufadhili wa aina yoyote. Pia muda ulikuwa mfupi, kwa hivyo utaratibu huu ukawa wa manufaa sana.

Pili, makosa yanapotokea katika utafiti katika utaratibu kama huu, ni rahisi sana kugundua na kurekebisha. Kwa sababu ya muda mfupi tuliokuwa nao, utaratibu huu ulifaa sana na nikaweza kumaliza kwa wakati uliohitajika.

Kwa sababu ya ukuruba mkubwa uliopo hasa kwa upande wa majina waliyopewa wahusika, nilishughulikia kila riwaya kikamilifu, moja baada ya nyingine kwa upande wa kupanga matukio yaliyodhihirisha matatizo katika jamii katika riwaya hizo.

Kazi ya ukusanyaji wa deta ulifanyika nyumbani. Haikuhitajika kwenda nyanjani hata kidogo.

3.2 Uchanganuzi wa Deta.

Katika uchanganuzi wa deta, mbinu iliyotumiwa ni mbinu ya kithamano. Nilichanganua deta iliyopatikana baada ya kupekua riwaya za Burhani. Nilitumia hii

mbinu ya kithamano kuainisha na kuchanganua deta za utafiti. Mugenda na Mugenda (1999) wanafafanua kuhusu mbinu ya kithamano kama inayorejelewa katika tafiti ambazo si jarabati; yaani zisizotegemea majaribio bali elimu na maarifa. Mbinu hii inasogelea kuwa matumizi ya mitazamo na makisio. Mtafiti anaweza kuteua uwanja wa mtalaa usiohitaji deta ambayo ni ya kijarabati.

Mathalani, tafiti zinazozingatia taratibu za upekuzi na mitaala ya kihistoria. Kwa hivyo, mbinu hii ya kithamano iliafiki sana utafiti huu kwani ulitumia utaratibu wa upekuzi wa yaliyomo katika kukusanya deta kutoka riwaya za Burhani, deta ambayo ni matukio katika riwaya hizo.

Katika utafiti nilipambanua deta kwa mpango na kitaratibu ili kuthibitisha nadharia tete zote mbili. Baada ya kukusanya deta kutoka riwaya, niliyaainisha na kuyapambanua matukio yaliyopatikana. Nilizingatia hatua zifuatazo:

(i) Kukusanya deta, kisha kuchuja na kuzipanga kulingana na aina ya tatizo na ya juhudi ama mikakati iliyotumiwa kulitatua tatizo hilo.

(ii) Kutumia mada ndogo kwa mujibu wa mawazo yaliyojitokeza katika kila riwaya, riwaya moja baada ya nyingine.

(iii) Kujadili na kutathmini matatizo yaliyomulikwa katika riwaya huku nikidondoa ushahidi kutoka riwaya husika, kisha namna ambavyo mwandishi anatumia mikakati mbalimbali katika utatuzi wa matatizo hayo. Nilikadiria uzito wa kila habari ama deta na ustahilifu, umuhimu, uthabiti,na kupatana (ama kutopatana) na nadharia tete za utafiti huu.

Baada ya kuzingatia hayo yote niliweza kuthibitisha nadharia tete ya kwanza na ya pili. Ili kuthibitisha nadharia tete ya kwanza, niliweza kubainisha matatizo mbalimbali aliyoyamulika Burhani katika jamii katika riwaya zake. Matatizo yaliyobainika ni kama vile, umaskini, mkengeuko, wivu, chuki, kudhibitiwa kwa mwanamke, ufisadi na kadhalika. Matatizo haya yalijengeka katika misingi ya migongano mbalimbali kama ilivyoelezwa katika 2.3.2 katika sura ya pili. Mathalani, migongano ya kiuchumi, kitabaka, kiaila, kiuana, kiumri, na kadhalika.

Nadharia tete ya pili, yaani kubainisha vile ambavyo Burhani anatumia mikakati mbalimbali kuyatatua matatizo yanayokabili jamii katika riwaya zake, nilichanganua kwa kina juhudi na mikakati aliyoweka mwandishi ili itumiwe katika kutatua matatizo yanayowakabili wanajamii na kurejesha tena hali ya salama na amani miongoni mwao. Mikakati mitatu iliyojadiliwa katika 2.3.3 ilibainika, hata hivyo, mikakati mingine ilitumika katika riwaya za Burhani, kama vile; kulizungumzia tatizo, yaani mhusika 'kutoa joto' lake, mapatano, mashauriano, kufadhiliana na kukubali kujirudi na kuanza maisha upya. Kwa kila hoja iliyotolewa, niliitetea na kuithibitisha kwa ushahidi uliodondolewa kutoka riwaya husika.

SURA YA NNE

MATATIZO YANAYOMULIKWA NA NAMNA YANAVYOTATULIWA

4.0 Utangulizi

Katika sura hii, deta niliyokusanya kutoka riwaya mbili za Burhani; *Mali ya Maskini* na *Mwisho wa Kosa* zinachanganuliwa. Deta ya utafiti ni matukio yanayodhihirisha matatizo katika jamii na namna mwandishi anatumia mikakati mbalimbali kuyatatua. Sura hii inapambanua matatizo yanayakabili jamii yaliyomulikwa na Burhani na namna ambavyo anatatua matatizo hayo. Fasihi inarejelewa kama kioo cha jamii na kazi mojawapo ya wasanii wa fasihi ni kujadili maswala nyeti na kupendekeza suluhisho kwa matatizo yanayoibushwa ama kuvyazwa na migongano mbalimbali katika jamii.

Burhani katika riwaya zake anamulika matatizo mengi katika mahusiano ya kijamii na kuonyesha vile ambavyo yanaweza kukabiliwa na kutatuliwa. Hata hivyo, ana dhamira kuu mbili. Katika *Mali ya Maskini,* anamulika jinsi umaskini unavyotokea kwa sababu ya mashindano kati ya biashara za matajiri ambazo zinastawi na zile ndogondogo ambazo zinafifia. Pili, katika *Mwisho wa Kosa,* anamulika tatizo la mgongano wa tamaduni; utamaduni wa kizungu na ule wa Kiafrika. Mbali na hayo, anamulika matatizo mengine ya kijamii kama vile ufisadi, ulaghai, ubadhirifu, matumizi mabaya ya mamlaka, ulaji rushwa na kadhalika. Kila tatizo linapofikia kilele chake, hali ya taharuki inatokea na suluhisho inatafutwa. Burhani anaweka mikakati mbalimbali ya kutatua matatizo hayo mbali na kuwafanya wale wanaoathiriwa kustahimili na kuwa na matumaini hadi pale ambapo utatuzi unafanywa na maisha yenye amani na salama kuanza tena.

Burhani ametumia majina yanayofanana kwa kiasi na ili kuondoa utata ambao unaweza kutokea, nitashughulikia kila riwaya, moja baada ya nyingine. Majina kama vile Ali, Keti, Zahara, Salama, Selemani, Hasani na Tatu yanatumika katika riwaya zote mbili. Aidha matatizo anayoyamulika na namna anavyoyatatua inaonyesha ukuruba, kwa hivyo, ili kufanya uchanganuzi wa kila riwaya kuwa bainifu, niliona ni muhimu kutochanganya uchanganuzi wa riwaya hizo. Kwanza nilishughulikia riwaya ya *Mali ya Maskini* kisha *Mwisho wa Kosa.*

4.1 MATATIZO YANAYOMULIKWA KATIKA KILA RIWAYA

4.1.1 *Mali Ya Maskini*

Mali ya Maskini (1981) ni riwaya ya kwanza aliyoandika Burhani. Kama mada yake inavyosema, riwaya hii inaangazia suala la umaskini, chanzo chake na matatizo mengine yanayoambatana nalo.Matatizo yaliyojitokeza katika riwaya hii ni:

4.1.1.1 Umaskini na Chanzo Chake

Burhani amemtumia mhusika Kadiri kumulika tatizo la umaskini katika jamii, chanzo chake, athari zake na namna ya kulitatua. Kadiri hapo awali alikuwa mtu wa kujiweza na hata aliweza kuwafaa watu wengine. Tunaelezwa kuwa, mzee Hasani alipoelemewa na umaskini, Kadiri alimsaidia. Badala ya kumpa pesa tu, aliona bora ampe kazi katika duka lake ili akidhi mahitaji yake. Hasani alitekeleza kazi hiyo kwa uaminifu hata baada ya wanawe kupata kazi na kuweza kumsaidia. Lakini wanavyosema Waswahili, ukiona mwenzio akinyolewa, chako tia maji. Kadiri alikabiliana na tatizo hilo la umaskini.

Wanavyosema Malotch (1976), Whitt (1982), ambao ni wananadharia wa nadharia ya mgongano kuwa katika miji, mashindano yanapotokea, washindi kila mara ni wenye mamlaka na pesa na washinde ni maskini na makundi madogo inajidhihirisha katika riwaya hii. Kadiri alianza kupata ushindani mkubwa kutoka kwa wafanyibiashara wakubwa, kwa hivyo, biashara ndogo ndogo kama ile yake zikaanza kufifia. Aidha, vitu vilianza kupanda bei, kodi za serikali zikapanda na karo za shule kuongezwa.

Maisha kwa Kadiri yanaanza kuwa magumu na watoto wake ikawa hawaelewi jinsi mambo yalivyobadilika. Ali, mwanawe mkubwa hafanyi kazi yoyote kumsaidia, anataka kutembea tu na anamtarajia babake ampe pesa za kujifurahisha. Zahara, bintiye kwa upande mwingine anataka avae vizuri kama rafikize. Mambo yanamlemea sana Kadiri na anamgombeza mkewe na kumlaumu kwa utovu wa adabu wa watoto. Anamwambia;

"Yote ni wewe. Unawaharibu hawa kwa kuwadekeza kwako, na kila nikikwambia hunisikii."(uk3)

Mkewe, Siti, anaelewa na kutomjibu, anamwachia 'atoe joto' lake lote kwani alielewa chanzo cha hamaki za mumewe sio tabia ya watoto bali mseto wa mambo mengi yaliyomkaa na kumkereketa kifuani na kumpa fursa ya 'kutoa joto' lake kungemtuliza na baadaye mwenendo wake kuwa wa kawaida. Siti anampendekezea Kadiri awaeleze watoto hali yake ya ufukara, anamwambia;

> "Ninaona afadhali uwaeleze hawa watoto hali yako ilivyo sasa..." (uk10)

Baada ya majadiliano machache, Kadiri anaona bora asubiri kidogo mpaka asikie Selemani atasema nini. Kadiri alitarajia kupata usaidizi kutoka kwa Selemani kwani alikuwa rafiki yake, waziri mwenye uwezo na kifedha. Wakati huo, Kadiri alikuwa katika hali ya mtafaruku, anamwambia mkewe;

> "Mpaka sasa hivi sijui mpango wa mwezi ujao, Ali na Zahara wanataka pesa za malipo ya shule na biashara haiendi vizuri..." (uk11).

Kadiri alienda kwa ofisi ya Selemani Kombo katika jumba la Wizara ya Biashara. Selemani anampa miadi waonane baadaye nyumbani kwake, kwa waziri. Kadiri anapomweleza Selemani tatizo lake nyumbani kwake na kuwa angependa amkopeshe pesa ili ainyanyue biashara yake, Selemani anampa ahadi ambayo inaambulia patupu. Kadiri anastahimili na kujitahidi kuendesha maisha yake. Aliwavumilia wadaku waliomsengenya kuwa amefilisika. Wengi ambao Kadiri aliwahi kuwasaidia hawakujitokeza kumfaa ila nduguye Bakari. Kwa kweli, mla nawe, hafi nawe ila mzaliwa nawe. Bakari aliyekuwa mtu mwenye uwezo mdogo, anamwendea Kadiri washauriane vile atakavyoweza kumfaa. Baada ya kutathmini njia kadhaa, Bakari anajitolea kuwalipia Ali na Zahara karo, aidha amchukue Zahara akae naye kwake. Hatua hii ya Bakari ilitatua tatizo la Kadiri kwa kiasi.

Shangaziye Kadiri pia anajaribu kuchangia katika kutatua tatizo la mpwa wake. Anamwambia kuwa ana akiba kidogo, shilingi mia tano ambayo ingemfaa, hata hivyo Kadiri anakataa na kumweleza kuwa alihitaji pesa kama hizo zaidi ya mara kumi. Siti, mkewe kwa upande wake anawapoza watoto kwa kuwaeleza ukweli wa mambo. Zahara anakubali kuenda kuishi kwa Bakari naye Ali anaanza kujifunza kazi ya ufundi katika karakana ya Bakari. Ali aliweza kupata pesa za kujisaidia yeye mwenyewe.

Aidha, baada ya kumaliza shule, hakukawia kupata kazi katika kampuni moja ya usafiri kama fundi, aliweza kumsaidia baba yake, Kadiri na pia kujiwekea akiba kila mwezi.

Msaada mkubwa anaoupata Kadiri ili kutatua tatizo lake la ufukara ni kutoka kwa rafikiye Hamisi. Hamisi alipomtembelea Kadiri katika duka lake, alistaajabu jinsi lilivyoishiwa na vitu. Anashauriana naye na anampa pesa zake azifanyie kazi, anunulie duka lake bidhaa na wagawe faida nusu bin nusu. Kadiri anafurahi sana na kumpa mkono Hamisi akisema;

> "Ninakushukuru sana sana Bwana Hamisi. Huwezi kujua namna gani ulivyonifurahisha siku ya leo kwa wema wako juu yangu..."(uk124).

Kadiri aliweza kujaza vitu katika duka lake tena. Ingawa matatizo mengine hayakuacha, kuibuka aliweza kukabiliana nayo kwa ujasiri zaidi kwa sababu hali yake kiuchumi ilianza kuimarika.

Mwandishi amemtumia Kadiri kama kielelezo cha wafanyibiashara wadogo katika jamii wanaofilisishwa na ushindani unaotoka kwa wafanyibiashara wakubwa. Hata hivyo, Burhani anaonyesha kwamba mtu hafai kukata tamaa na kutamauka bali alikabili tatizo hilo kwa ustahamilifu huku wanajamii, hasa aila yake na marafiki wakichangia katika kumnasua kutoka tatizo hilo. Kwa kutumia mfano wa Kadiri, Burhani pia ameonyesha kuwa kila msiba una mwenziwe na kila mtu anapoathiriwa anafaa kukabiliana nayo kwa ujasiri na kwa ustahamilifu na hatimaye ataongoka.

4.1.1.2 Mkengeuko na Uhuru wa Vijana.

Mkengeuko ni hali inayotokana na kule kukengeuka, yaani, kupotea njia kwa kutozingatia mila na desturi za jamii. Kama ilivyoelezwa katika misingi ya nadharia, 2.3.3, wananadharia wa nadharia ya mgongano wanaeleza baadhi ya aina za mkengeuko kuwa ni ulevi, kutumia madawa ya kulevya, ugomvi wa kifamilia, uasherati na kadhalika. Katika *Mali ya Maskini,* Burhani amemtumia mhusika Ali ambaye ni kijana kama kielelezo cha vijana wanaohisi haja ya kuwa mbali na wazee wao na kuwapinga ili kujihakikishia uhuru wao kwa kiasi fulani katika maisha yao. Vijana kama hawa wanaishia kutenda vitendo vya upotofu na ukengeushi.

Burhani anaonyesha kuwa hatima ya vijana kama hawa wanaokaidi mila na desturi na kujiingiza katika mambo ya uhalifu ni kufungwa jela ili wazinduke na kujirudi.

Ali ni kijana aliyeingilia anasa na kuwa mbadhirifu. Alitumia pesa kwa fujo na bila mpango na alifanya urafiki na msichana anayeitwa Keti. Keti alisifika sana katika kucheza dansi. Ali alitumia pesa zake kumfurahisha Keti na kumnunulia zawadi nyingi kama vile sahani za santuri na redio aina ya *Stereo*. Aidha alimpangishia nyumba na kuchukua vyombo kwa mkopo ili kuipamba nyumba hiyo. Keti anakuwa kupe kwa Ali na anafikia kiwango cha kutomtaka awasaidie wazee wake, anamchochea awachukie, anamwambia;

"...tena na hao wazee wako. Robo ya mshahara wako takribani unawapa wao. Kwa nini? Unafikiri watu wote wanafanya hayo kwa wazee wao?

(uk 52).

Ali alijitaabisha sana ili kukidhi tamaa za Keti za starehe na vitu vya anasa. Hatimaye anashawishika kufanya kazi ya magendo ili kupata pesa zaidi za kulipia madeni mengi yaliyomzunguka na kumfurahisha Keti. Ali alifanya kazi hiyo ya kusafirisha bidhaa za magendo kila Ijumaa usiku na kurejea siku ya Jumapili usiku na pesa mkononi. Hata hivyo, madeni yake yalizidi badala ya kupungua kwa sababu ya tamaa za Keti zilizozidi kuongezeka.

Tamaa za Keti zinamfanya aingilie urafiki na askari anayeitwa Hasani, urafiki wao unakua hadi Keti anashawishika kufichua siri ya Ali ya kujihusisha na magendo ili kumpa Hasani sababu ya kupandishwa cheo. Familia ya Ali ilianza kuingiwa na wasiwasi. Baada ya kufanya uchunguzi, Kadiri anagundua kuhusu sifa mbaya za Keti. Aidha rafiki yake mmoja aliyekuwa askari anamfichulia na kumwonya kuhusu tabia ya Ali kujiingiza katika magendo. Ili kutatua matatizo ya Ali, Kadiri anaitisha mkutano wa dharura ambapo wanaazimia kumtafutia na kumwoza mke. Kadiri pia anachukua fursa hiyo kumwonya Ali dhidi ya kufanya magendo kwani palikuwa na mitego amewekewa na angenaswa asingetahadhari. Ali alikoma misafara hiyo ya magendo na mipango mibaya ya Keti ikaambulia patupu. Ali hatimaye aliozwa msichana aliyeitwa Alama, bintiye Usi. Harusi iliandaliwa na Ali alianza maisha mapya.

Hata hivyo, mchovya asali hachovyi mara moja. Ali hakumsahau Keti, aliendeleza urafiki wao licha ya ugomvi na vita vilivyokuwepo kati yao. Alama alivumilia sana wakati wote Ali hakuonekana nyumbani.

Ali alifikia kiwango cha kuiba vyombo vya mkewe vya dhahabu na feruzi ili kumfurahisha Keti na kumdanganya kuwa aliuza ili 'kuifufua' duka la babake. Kilele cha mgogoro huu ni wakati ambapo Ali na Keti wanapigana na Keti anateleza na kujiumiza vibaya. Vita hivi vilisababishwa na kiburi cha Keti ambaye alimjibu vibaya Ali aliyetaka kujua ameagana kutembea na nani, alimjibu;

> "Unanitakia nini? Inakuhusu nini wewe...Huna haki yoyote ya kunipa amri..."(uk135).

Ali anapomwambia anayo haki ya kumwamrisha, anamfokea;

> "Nenda huko. Nenda ukakae na huyo kizuu chako. Nilikwambia zamani ukae hukohuko..."(uk 135).

Keti alilazwa hospitalini na Ali akatiwa kizuizini. Siku za mwizi ni arobaini na inafika siku ya arobaini kwa Ali. Ali, kwa sababu ya kutozingatia mila na desturi za wazee wake, anafundishwa na ulimwengu. Mwandishi anaonyesha kuwa asasi ya jela hutumiwa kuwarudi vijana mfano wa Ali.

Wazee wake Ali na wakwe zake wanashirikiana kumsaidia Ali. Usi, babake Alama anakuwa wa manufaa kwa sababu alikuwa na elimu ya sheria. Bakari anamtafuta wakili na anapopatikana, Kadiri anagharamia kwa kukopa pesa kwa rafiki yake Hamisi. Zahara na Bakari wanakubali kutoa pesa kiasi fulani kila mwezi ili kulipia deni hilo. Ali alifikishwa mahakamani kwa mashtaka yaliyomkabili. Kesi alichukua muda na ilipomalizika, Ali aliachiliwa kwa sharti kuwa alipe gharama na hasara yote aliyopata Keti. Familia yake ilifurahi na Alama akarejea. Baada ya kushauriwa na mamake, Ali akabadilika, akaomba msamaha na kukata kauli kutorejea tena kwa Keti. Maisha yanaanza upya yakiwa ya imani na masikilizano.

Burhani ameonyesha kuwa tatizo la mkeugeuko wa vijana linapotokea linakuwa vigumu kulitatua hasa pale ambapo vijana wanang'ang'ania kujihakikishia uhuru wao. Njia ya kuwarekebisha vijana watundu mfano wa Ali inakuwa kutiwa kizuizini na

kushtakiwa. Burhani, anahimiza aila ya kijana aliyejiingiza katika vitendo vya uhalifu na upotofu wajitolee bila kuchoka kumsaidia na hatimaye wataweza kumwokoa.

4.1.1.3 Matumizi Mabaya Ya Mamlaka

Matumizi mabaya ya mamlaka yanadhirishwa kupitia mhusika Seleman Kombo ambaye ni Waziri wa Biashara. Kumekuwa na kashfa nyingi zinazowarejelea mawaziri na watu wengine wenye mamlaka wakiwa wamejihusisha na matumizi ya nafasi yao ili kufaidi nafsi yao, hasa kwa kuwalaghai wasichana wadogo ili kuwatumia kimwili. Katika *Mali ya Maskini*, Burhani amemtumia Selemani kama kielelezo cha viongozi wa aina hiyo. Zahara na Yusuf ni vijana wanaoathiriwa na tabia hii lakini vijana hawa wanakabiliana na tatizo hili bila kulegeza msimamo wao.

Zahara alipokuwa akitafuta kazi, Selemani alimpata njiani akalisimamisha gari lake karibu naye na kumshawishi aingie garini. Selemani alidai kuwa rafiki mkubwa wa babake na kuwa alikuwa tayari kumsaidia Zahara kupata kazi. Siku ya pili, Zahara anafika afisini mwa Selemani ili apewe nafasi ya kazi. Tabia ya ufisadi ya Selemani inaanza kudhihirika kwa sababu nafasi iliyopo ni moja tu na anamwambia Nasoro, mkuu wa kuangalia wafanyikazi, atangaze magazetini ili ujanja wake usitambulike. Anamwambia apeleke mambo kama desturi. Anamwambia Nasoro;

"Aah, ipelekwe kama desturi...lakini Bi.Zahara hapa atakapoliona
tangazo hilo atatuletea ombi lake"(uk65).

Zahara anaposhangaa jinsi atakavyopata kazi hiyo miongoni mwa watafuta kazi wengi, Selemani anampoza;

> "...usitie wasiwasi, kwa sababu lazima sisi tufuate njia fulani zilizowekwa kisheria. Lakini sasa nimekwisha zungumza na Nasoro na yeye analijua jina lako, kwa hivyo utakapoleta ombi lako, litakubaliwa tu mwanzo" (uk66).

Baada ya Zahara kupeleka maombi yake, Selemani alianza kufanya urafiki naye. Siku moja, Ali aliwaona wakinywa soda katika mkahawa mdogo, alipowauliza watumishi kama walimjua mtu aliyekuwa na Zahara, mmoja alimjibu;

> "Mwenzangu, yule ni mmoja katika waheshimiwa, waziri....kila siku anabadilisha wake ,inaonyesha kama anatafuta mwingine. Sijui huyu atakuwa wa ngapi?"(uk68)

Maoni haya ya mtumishi hotelini yanaonyesha kuwa Selemani amekuwa akionekana pale na wasichana tofautitofauti. Jioni siku hiyo, Ali anamwuliza Zahara kuhusu tukio kilo lakini anaonekana mkembe kwa laghai za 'mababa – sukari' kama Selemani.

Ali anachukua hatua na kumweleza Kadiri, baba yao kuhusu tukio hilo. Kadiri anamwonya Zahara asifuatane tena na Selemani. Hata hivyo, Selemani aliendelea kumwita Zahara ofisini mwake mara nyingi hadi wafanyikazi wenzake wanamfanyia mzaha, wanambandika jina 'rafiki ya mheshimiwa'. Urafiki unaota kati ya Zahara na kijana aliyeitwa Yusuf. Kunaibuka ushindani kati ya Yusuf na waziri. Hali hii inazua migogoro kazini, baadhi ya wafanyikazi wanaanza kumshutumu Yusuf kuwa anatembea na rafiki ya mkubwa, mheshimiwa. Kwa sababu ya migongano hii, Yusuf anapata uhamisho katika Wizara ya Fedha, Selemani alifanya hivi ili apate nafasi nzuri ya kumtongoza Zahara.

Selemani anaamua kuchukua hatua ya haraka kupeleka posa kwa Kadiri akifikiri cheo na uwezo wake ungemrahisishia mambo. Kadiri anasisitiza ni sharti ashauriane kwanza na wazee wengine na pia Zahara mwenyewe. Katika mkutano aliouitisha Kadiri, anawaeleza kuhusu tabia yake ya kuoa, anamwambia;

> "Anaye mke wa kwanza, mke mkubwa ambaye naye. Aliwahi kuoa tena mara mbili tatu; vijana, watoto kama Zahara Lakini amewaacha" (uk93).

Kutokana na maelezo hayo na mengine kuhusu Selemani, walikubaliana kuwa hapakuwa na haraka ya kumwoza Zahara kwani bado angali mdogo hasa kwa mzee kama Selemani. Aidha, Kadiri anamshauri Zahara ili kuona msimamo wake. Zahara anapokataa na kusema hampendi kabisa huyo waziri, Kadiri anajihisi kama ameondolewa mzigo.

Suluhisho kwa tatizo hilo ambalo lilikuwa limeelemea Zahara na familia yake linatokea wakati ambapo Yusuf anamtumia mzee wake mmoja kupeleka posa kwa Kadiri. Kadiri anawaita wazee wa upande wake ili washauriane, wote walifurahi na wakamwachia Zahara afanye uamuzi wake wa mwisho. Zahara hakuwa na upinzani wowote na harusi inapangwa. Harusi inakuwa ya kufana na pande zote mbili zilifurahia sana. Yusuf na Zahara walikodi nyumba yao na kuhamia. Zahara alitafuta kazi nyingine

ili kujiepusha na waziri Selemani. Anapata kazi katika kampuni moja iliyotengeneza na kuuza vitu vya nyumbani. Maisha yake yanakuwa tulivu tena, yenye amani na salama.

Burhani amelimulika tatizo hili la matumizi mabaya ya mamlaka kama linalohitaji wale wanyonge, kwa mfano, vijana na wanawake wawe jasiri, walikabili moja kwa moja bila ya kutahayari. Yusuf anamkabili Selemani bila ya woga na anaendelea na mipango yake kumwoa Zahara. Zahara naye kwa upande wake anakataa kuitikia mipango mibaya ya Selemani. Watu wenye mamlaka na mali kama Selemani wanapata funzo kuwa, utajiri na ukubwa kazini si kila kitu, si muhimu, lililo muhimu ni utu.

4.1.1.4 Wivu na Chuki katika Familia

Burhani amelimulika tatizo hili kwa kiasi. Anaonyesha kuwa migongano katika familia/aila hutokea pale ambapo mtoto wa ndugu analetwa ili kulelewa pamoja na wengine katika nyumba. Kwa tatizo kama hili, anaonyesha kuwa muhimu ni kustahimili hadi mambo yatakapopoa, pia mashauriano yanapewa umuhimu. Wanaoendeleza tatizo hili hasa ni wanawake, kama vile Imani ambaye ni mke wa amu wa Zahara. Imani anamwonyesha Zahara chuki na wivu sana wakati ambapo analetewa amlee pamoja na watoto wake.

Hartman (1981) anaiona aila kama inayoeleweka zaidi kama uwanja wa mashindano bali si kwa misingi ya mahusiano ya kihisi au ya kiukoo. Tunaona ukweli wa makisio haya ya nadharia ya mgongano katika riwaya ya *Mali ya Maskini* wakati ambapo Bakari anamchukua Zahara, binti wa nduguye, Kadiri kwake ili amlipie karo na amtunze, mkewe, Imani hafurahishwi, anamwonyesha chuki. Mwandishi anatueleza vile Zahara alimwona Imani siku ya kwanza, anasema;

> "...jicho lake lilimwangukia mke wa Bakari; alipoona namna mwanamke huyo alivyomwangalia kwa chuki, moyo wake ulimpinduka..."(uk42).

Imani alimchukia Zahara kwa sababu hakumtaka mumewe amlete nyumbani mwao, aliona familia ya Kadiri ilikuwa na vitu vingi kuliko wao na hakuona sababu ya kuwasaidia, anamlalamikia Bakari;

> "...huyo Kadiri ana vitu vingi zaidi ya tulivyo navyo sisi? (uk31).

Imani alimsingizia Zahara makosa mengi sana, anavyoeleza mwandishi, kulikuwepo na 'vita baridi'. Zahara analazimika kuhama kutoka chumba chake kwenda ukumbini na hatimaye uani ili aweze kusoma vitabu vyake. Siku moja alishtukia Imani amevipiga teke na kuvitawanya vitabu vyake kila mahali na kumfokea kwa hasira;

> "Vitabu, vitabu kila pahala! mtu hapati hata pa kuweka mguu. Vitabu gani navyo? Sikupata kuona mtu akasoma uani tena! ".

Ili kupunguza ama kuondoa mgogoro huu, Zahara alitumia busara na badala ya kushindana na Imani, alimwambia Bakari kuwa masomo yamekuwa mengi na magumu na angependa kila siku baada ya kurudi kutoka shule, akapitisha masaa kidogo katika maktaba, au kuwa na wenzake ili wadurusu pamoja. Zahara hakutaka kumshutumu Imani kwa sababu kungezuka mgogoro zaidi, Bakari anapomwambia mbona asisomee hapo nyumbani anajitetea;

> "...Kwa kweli vipo vitabu fulani fulani ambavyo ninavihitajia na nitaweza kuvipata huko, na tena tulikuwa pamoja tunaweza kufahamishana na kuelewa kwa wepesi zaidi?" (uk43)

Bakari alimkubalia na kwa kiasi aliweza kutuliza mgogoro uliokuwepo. Kila aliporudi magharibi na baada ya chajio, aliosha vyombo. Imani hata hivyo aliendelea kulalamika na siku moja hakupika chajio na akawanunulia wanawe chakula. Zahara alipofika jioni hiyo, anakuta hakuna cha kukila, fauka ya hayo, alionyeshwa madharau, Zahara anarudishiana maneno na Salama, ubishi ambao unaishia mapigano. Wapita njia wanawaamua na kumwita Imani.

Bakari alipoingia jioni na kuarifiwa kuhusu ubishi huo, anamlaumu Imani kwa kutowajibika na anajipa jukumu la kuwanasihi na kuwapangia kazi watoto; Salama, Tatu na Zahara. Wanakubali kufanya kazi kwa zamu. Zahara akaendelea kustahamili na kukabiliana na chuki alizoonyeshwa. Hatimaye, Zahara anafanya mtihani wake na kupasi vizuri. Kila mtu alifurahia matokeo ya Zahara na kumtuza zawadi , isipokuwa Imani.

Zahara anapata bahati kuajiriwa kazi katika ofisi moja ya waziri Selemani. Zahara wakati mmoja anajipa ujasiri kumwelezea babake kuhusu chuki alizoonyeshwa na Imani, mkewe Bakari, hapo, alipata 'kutoa joto' lake anavyosema mwandishi. Kadiri

alimshauri aendelee kustahimili na punde, kilele cha mgogoro huu inafika pale ambapo Zahara anaozwa kwa Yusuf, kijana ambaye alimpenda. Harusi yao ilifana sana na kila mtu alifurahia ila Imani lakini Zahara hakuzijali chuki zake tena. Yeye na mumewe walikodi nyumba yao na kuhamia. Tatizo la Zahara linafikia hatima yake. Kwa kutumia mfano wa Zahara, mwandishi anapendekeza kuwa, katika kutatua migogoro ya kifamilia, kunahitajika ustahamilifu kwa yule au wale wanaoona wanadhulumiwa. Aidha, mashauriano na maamuzi yenye busara yanahitajika, vile ambavyo Zahara na Bakari walifanya. Wangefanya kinyume kwa kuendeleza ubishi, vita vikali vingezuka na madhara yangetokea.

Katika riwaya ya *Mali ya Maskini*, tumeona vile ambavyo Burhani anamulika na kutatua matatizo katika jamii. Katika riwaya hii, ameangazia tatizo la umaskini unaotokana na mashindano ambayo kwayo, biashara za matajiri zilistawi na zile ndogondogo, kama vile ya Kadiri zilififia. Tumeona pia tatizo la uasi unaotokana kwa vijana kutaka uhuru, matumizi mabaya ya mamlaka na migogoro ya kifamilia.

Katika kuyatatua matatizo haya, Burhani amependekeza ustahamilifu wakati wa kukabiliana na matatizo yanayoibuka, kufanya mashauri, kufanyiana hisani na njia hizi zote zikikosa kusaidia, kuna asasi ya jela na mahakama. Muhimu ni kwamba, hatima ya kila tatizo ni maisha yenye amani na salama.

4.1 2 *Mwisho wa Kosa*

Riwaya ya *Mwisho wa Kosa* ni ya pili ya Burhani. Dhamira kuu katika riwaya hii ni kumulika tatizo la mgongano wa kitamaduni na kuonyesha madhara yanayotokana na kutozingatia matakwa ya mila na desturi za jamii. Burhani anaangazia mgongano kati ya utamaduni wa Kiafrika na ule wa Kizungu. Anamtumia Monika, bintiye mzee Mhaji kama kielelezo cha vijana ambao wanakwenda ng'ambo na kuiga na kukoleza 'uzungu.' Monika aliporudi kutoka masomoni anaonekana tofauti na anashindwa kuzingatia misingi na matakwa ya utamaduni wa wazee wake, Anatoroka nyumbani kwao lakini kule nje anakabiliwa na ulimwengu uliojaa walaghai, hali ambayo hatimaye inamfanya atambue kosa lake na kujirudi na kurudi nyumbani.

Kama anwani ya riwaya hii inavyoelekeza, tunatarajia kuona kosa na mwisho wake. Monika anapojirudi na kurejea nyumbani kwao, anatambua kosa lake na linakuwa mwisho wa kosa. Mbali na tatizo la utamaduni, kuna matatizo mengine mengi kama vile wivu, chuki, kudhibitiwa kwa mwanamke katika ndoa, ufisadi na kadhalika. Kwa hivyo, kosa si moja bali kuna makosa mengi, kila kosa likiwa na mwisho wake. Makosa yanayomulikwa ni matatizo yanayovyazwa na migongano; migongano hiyo inapofikia kilele, suluhisho la kutatua tatizo linatafutwa na mwisho wa kosa hilo unatimia.

4.1.2.1 Mkengeuko na Madhara yake

Tatizo la mkengeuko lilijitokeza pia katika riwaya *Mali ya Maskini*. Kama nilivyoeleza, mkengeuko unatokana na hali ya mtu kupotoka kwa kutozingatia matakwa ya kijamii. Nadharia ya mgongano ilitoa mifano ya mkengeuko kama vile; ulevi, ugomvi wa kifamilia, kutumia madawa ya kulevya, uasherati na kadhalika. Katika *Mwisho wa Kosa,* hali hii inajitokeza kwa jinsi mbili, kwanza kama kuasi utamaduni na pili kama matumizi ya madawa ya kulevya.

4.1.2.1.1 Kuasi Utamaduni

Tatizo kuu linaloangaziwa katika *Mwisho wa Kosa* ni kuasi utamaduni na madhara yanayotokea wakati ambapo vijana wanakaidi na kutenda kinyume cha matakwa ya kijamii. Tatizo hili linakurubiana na tatizo la mkengeuko na uhuru wa vijana ambalo lilijitokeza katika riwaya ya *Mali ya Maskini,* tofauti tu ni kuwa, Ali anakia mipaka ya kukaidi mila na kuingilia matendo ya kihalifu. Katika *Mwisho wa Kosa,* mwandishi ametumia mfano wa Monika, bintiye Bw. Mhaji. Monika alipokuwa akirejea kutoka masomoni ng'ambo, aila yake na marafiki walienda kumpokea katika uwanja wa ndege kwa furaha kuu. Hata hivyo, Monika wanayempokea katika uwanja wa ndege ni tofauti kabisa na yule waliyemjua. Alionyesha 'uzungu' kimavazi, kimapambo na kitabia. Hakuonyesha uchangamfu kwa wale waliokwenda kumpokea ila alitaka waondoke kwa haraka. Wanapofika nyumbani, Monika anadharau kila kitu anachoandaliwa, Salama, msichana aliyelelewa pamoja naye anashangaa sana. Kila

mara wanapozungumza, Monika alipenda kuanza kwa maneno kama 'Kule Ulaya, sisi hatufanyi hivi...' au 'Kule Ulaya, watu hawapendi mambo kama haya.'

Monika alipopata kazi, anakoleza ubinafsi na uchoyo, hakuwasaidia wazee wake hata chembe. Wakati mmoja, mamake Bi Tatu anaenda kwa Bi. Riziki ili kukopa pesa alizohitaji ili aende kuhudhuria harusi ya nduguye huko shambani. Kinaya ni kwamba, Salama, rafikiye Monika anakubali kutoa nusu ya akiba yake, shilingi mia nne ilhali alipata mshahara mdogo kuliko Monika. Analalamika mamake kwa kusema;

> 'Lakini Monika anafanya kazi!...' 'na unajua mshahara wake kiasi gani? Anapata mara tatu zaidi yangu mimi.' (Uk.7).

Bi. Riziki anaongezea;

> '... Anapata pesa hizo zote lakini unajua kuwa hawasaidii wazee wake kwa chochote!'

Maoni ya wahusika hawa yanatuonyesha jinsi ambavyo Monika aliingiwa na ubinafsi na hata kuwasahau wazee wake waliomzaa na kumlea, tabia hii yake ni kinyume kabisa na mila na desturi za Kiafrika.

Ukengeushi wa Monika unadhihirika pia wakati ambapo anaudharau na kuumwaga uji wa Bi. Keti. Siku moja, Bi.Tatu hakuwepo na nduguze Monika wakawa wamebanwa na njaa na wakaenda kwa Bi. Keti kuomba wapewe uji wa mkopo ili mama yao akirudi aje akalipe. Baada ya kunywa, Bi. Keti aliwatilia ili wampelekee dada yao, Monika, ambaye alipopewa, aliukunja uso wake na kusema;

> 'Nani kakwambia nataka uchafu huo. Nenda kaumwage huko!' (uk.11)

Baada ya maneno hayo, Monika aliumwaga huo uji, kitendo ambacho kilimsinya Bi. Keti na ugomvi ukatokea baina yao. Bi Keti anashindwa kujizuia na anamzaba makofi. Monika anaudharau uji ambao ulitumiwa kumlea alipokuwa mdogo. Bi. Keti analalamika kwa kusema;

> "... Ndio mchafu, huwezi kuunywa leo? Umesahau kama uji ule ndio uliokulea wewe mpaka ukawa hivyo, eh? ...' (uk. 11).

Wazazi wake Monika waliporudi, walikuta ugomvi ule unawangojea. Walionyesha utu kwa kufanya kila jitihada ya kupooza na kumwomba radhi Bi. Keti.

Monika aliendelea na vitimbi vyake pale anapozusha zogo nyumbani kwao kwa sababu wazee wake walimnasihi asivunje uchumba kati ya Rashid na Salama. Monika anakaidi nasaha za wazee wake na hata kumkaripia babake, tabia ambayo inamfanya Bw. Mhaji amzabe kofi. Monika anajibu kwa kiburi;

> 'Hayo mimi hayanihusu hata kidogo. Sijui mnaishi vipi? Lakini hii ni karne ya ishirini, na dunia ya sasa kila mtu na nafsi yake tu. Kwanza uchumba huo ...wamepangiwa tu na wazee wao.' (Uk. 58).

Tabia ya Monika ilikuwa ikitishia kuvunja udugu, ujirani na wema uliokuwepo kati ya familia hizo mbili. Anaamua kutoroka nyumbani kwao kwenda kuishi kwa Rashid. Ubinafsi na unyeti wake unaonekana katika usemi wake;

> 'Na mimi nitaondoka nikuachieni hiyo nyumba yenu. Madhali nina pesa sitakosa pa kukaa. Kwanza nyumba gani nayo! Mtu hata anaona haya kuleta wenzake humu ndani.' (Uk. 58).

Monika aliendelea kujizamisha katika starehe na anasa wakati alipokuwa mjini.Tabia hizi zinamwudhi Rashid wakati anafanya urafiki na walaghai. Kilele cha tatizo la Monika ni pale ambapo analaghaiwa na waziri, Bw. Matata. Monika anazuzuika na kuona kama angeolewa na waziri, ambaye alikuwa umri wa babake. Tunaelezwa kuwa alikuwa na tabia ya kuoa kila mara. Nyumba anayoishi Monika inapokosa kulipiwa kodi kwa muda, mwenye nyumba anafika na anapokosa kodi yake, analalamika;

> '... Ala! Amezoea tu! Siyo anitolee watu! Katika nyumba akichukua mapesa akioa kila siku na kodi ya watu asilipe.'(uk252)

Ukweli unamdhihirikia Monika wakati ambapo wenzake kazini wanamfanyia mzaha. Wanapomuuliza ikiwa ataenda harusini, Monika anafikiria ni harusi ya Rashid, anasema kwa maringo;

> 'Kwani huyo Rashid ndiye nani? Wataniona nitakapokuwa mke wa Waziri!'(uk254)

Lakini anapofumbuliwa ukweli kuwa harusi ni ya mheshimiwa Bwana Matata, haamini ameambulia patupu. Anaingiwa na mtafaruku mkubwa. Monika anaamua kutafuta njia ya kutatua mtafaruku huo. Anakwenda kwa Waziri wa Kilimo, Bw. Selemani huku akitiririkwa machozi. Kwanza anataka kuhakikishiwa kuwa habari aliyopata kutoka wenzake ni kweli, Selemani anamwarifu kuwa Bw. Matata anamwoa msichana mdogo wa miaka kumi na sita kwao vijijini. Monika anafunguka macho, anatambua kuwa alikuwa amezuzuka na mbio zake za sakafuni zimefika ukingoni. Kwa kweli, ng'ombe akivunjika guu malishoni hurudi zizini.

Mwandishi katika utatuzi wa tatizo lililomkabili Monika anawatumia wahusika wazee: Bw. Selemani, Bw. Selele na Bw. Mhaji, babake Monika. Bw. Selemani anampeleka kwa Bw. Selele ambaye anajitolea kumlipia Monika kodi ya nyumba badala ya mheshimiwa. Bw. Selele anampigia simu Bw. Mhaji ambaye alikuwa pia rafiki yake. Wazee hawa wanalizungumzia tatizo la Monika na baada ya mashauriano marefu, Bw. Mhaji anapokea bintiye na kumwelezea masharti, mojawapo ikiwa ni kumwoza pindi mume atakapotokea. Monika anajisikitikia na kukiri kuwa alikuwa amejifedhehesha vya kutosha. Hatimaye, Monika anaozwa kwa mwana wa amu yake, Shaabani. Hakupata fursa hata kidogo ya kufikiria ikiwa kweli anampenda au la. Mipango yote ya harusi inafanywa na anakuwa mke wa mtu.

Burhani anamsawiri Monika kama mwana mpotevu katika Bibilia ambaye anahangaishwa na ujana na wakati ambapo mambo yanamharibikia, anarejea kwao nyumbani na kuomba msamaha na kuanza maisha upya. Namna anavyotatua matatizo Burhani ni kinyume kabisa na wanavyofanya wasanii wengine kama E. Kezilahabi. Kezilahabi katika *Rosa Mistika* kwa mfano hampi Rosa fursa ya kuanza upya wakati matatizo yake yanafika ukingoni, badala yake, suluhisho linakuwa kifo. Kazi ya Burhani haiishii utamaushi bali mwanzo mpya wenye matumaini.

4.1.2.1.2 Matumizi ya Madawa ya Kulevya

Burhani amemulika tatizo la matumizi ya madawa ya kulevya miongoni mwa vijana. Mkengeuko huu si tofauti na ule wa Ali Kadiri katika riwaya ya *Mali ya Maskini*. Hili ni tatizo sugu hasa katika jamii ya kisasa. Vijana wengi hujiingiza katika

matumizi ya madawa ya kulevya wakitumainia kuimarisha utendaji wao katika nyanja kama vile masomo na riadha. Katika *Mwisho wa Kosa*, Burhani amemtumia Ali kama kielelezo cha vijana wanaothiriwa na kupotoka kwa sababu ya kutumia madawa ya kulevya. Awali, Ali alikuwa kijana mwenye jitihada na kiongozi wa chama cha wanafunzi chuoni. Wakati ulifika ambapo Ali alipoteza wakati wake mwingi katika mambo ya siasa hata babake akaalikwa chuoni na kuambiwa amuonye azingatie masomo.

Tabia hii ya Ali iliwatia wasiwasi walimu wake ambao walijaribu kumnasihi aache mwenendo wake na azingatie masomo yake kama hapo awali. Ali alikuwa ametia masikio yake nta na siku moja akatanabahi kuwa mtihani umekaribia na hakuwa amesoma hata chembe. Alianza kusoma bila kusita lakini bado aliona wakati hautoshi. Ali anapatwa na kishawishi na kunaswa katika mtego wa madawa ya kulevya pale ambapo anamkuta kijana mmoja katika basi ambaye anamwelezea kuhusu dawa ambazo angezitumia ili kuondoa usingizi kabisa, anamwambia;

> '. Usitie wasiwasi, sikiliza. Rafiki yangu mmoja anafanya kazikatika duka la madawa na ameniambia kuwa kuna vidongeambavyo ukivimeza vinatoa usingizi kabisa!...'(Uk. 110.)

Ali anaangukia mtego na kijana huyo ambaye anamuuzia kijichupa cha dawa. Ali anavitumia vidonge hivyo vile alivyoagiziwa na kwa kweli usingizi ulimpaa. Ali alisahau kuwa usingizi una umuhimu mkubwa katika kupumzisha akili. Madawa haya hatimaye yalimfanya Ali kuporomoka darasani, alipopata fahamu alikuwa hospitalini.

Kwa mujibu wa sheria za chuo, Ali alikuwa amefanya kosa kubwa sana. Aliadhibiwa kwa kufukuzwa chuoni. Ali anasononeka sana na kuanza kutafuta kazi. Wazee wake, hasa babake anamnasihi akakubali hali yake na asione kama ni mwisho wa kila kitu. Rashid pia anamtembelea na kumnasihi na kumsaidia kutafuta kazi. Hatimaye Ali anapata kazi kupitia Karne, rafikiye Rashid katika kampuni ya gazeti moja mashuhuri. Bahati ya Ali haikomei hapo, baadaye anapata kazi katika kiwanda cha kutengenezea magari aliposaidiwa na Alison, rafikiye Rashid. Maisha ya Ali yanaanza kuwa mazuri na anakuwa mtu wa kutegemewa.

Ali wa *Mwisho wa Kosa* kwa kiasi anakurubiana na Ali Kadiri wa *Mali ya Maskini.* Burhani anaonyesha kuwa, japo kijana anaweza kujikuta katika utata kama aliojikuta Ali, bado ana fursa ya kuanza upya na kufaulu maishani. Muhimu ni kugeuza mwenendo wake. Katika kutatua tatizo lililomkumba Ali, aila yake na marafiki walishirikiana kumnasihi na kumtafutia kazi ya kumwezesha kuanza upya. Ali hatimaye anakuwa mtu wa kutegemewa.

4.1.2.2 Ufisadi

Burhani katika riwaya ya *Mwisho wa Kosa* amemulika tatizo la ufisadi katika jamii. Ufisadi umekuwa tatizo sugu katika jamii na aghalabu viongozi watasikika wakihimiza vita dhidi ya ufisadi. Tatizo hili hujitokeza katika maofisi ya serikali, makampuni, shuleni, mahospitali,na kadhalika.Dhana hii ya ufisadi hurejelea matendo maovu hasa yale yanayoishia kutia hasara mtu fulani ama umma. Katika riwaya ya *Mwisho wa Kosa,* aina za ufisadi tunazoona ni ulaji rushwa na matumizi mabaya ya mamlaka.

4.1.2.2.1 Ulaji Rushwa

Burhani katika *Mwisho wa Kosa* amemulika tatizo la ulaji rushwa, tatizo ambalo limekithiri sana katika jamii, kwa mfano katika idara ya polisi, vyuoni, maofisi ya serikali, forodhani na kadhalika. Katika riwaya ya *Mwisho wa Kosa*, Burhani anamtumia Rashid kama mfano wa maofisa katika ofisi za umma ambao wanashawishika na kunaswa katika mtego wa ulaji rushwa. Rashid alifanya kazi yake kwa jitihada na uaminifu. Alipata mshahara mzuri. Wakati mmoja alipokuwa akikagua maombi ya makampuni yanayotaka kupewa kandarasi za serikali. Alison, wa kampuni moja ya Kijapani aliandaa karamu na kumwalika Rashid ili amteke bakunja aipendelee kampuni yake. Alison anamkumbusha Rashid kuwa atapata sehemu yake; yaani mlungula. Rashid, bila kujua anakuta amenaswa katika mpango wa Alison.

Baada ya kutambua kwamba amenasika katika huo utando wa mlungula, Rashid anajuta, anajiona haini, mwizi na mwenye pupa. Anaingiwa na hali ya mtafaruku kwani anaona hawezi kurudi nyuma ila kuendelea kutimiza matakwa ya

Alison. Swali linalomtatiza ni Je, Akipatikana? Mkutano wa kutoa kandarasi unapofanywa, Rashid hakuwa na budi kuchagua kampuni ya Alison. Baada ya tukio hili, uvumi unazuka ofisini kuhusu Rashid kupokea mrungura kutoka kampuni moja ya Ujapani. Habari hizi zinamtia wasiwasi sana. Musa, rafikiye anafika ofisini kumwonya Rashid kuhusu yale yanayoendelea na kwamba kuna watu wanaotamani cheo chake.

Rashid anaanza kutafuta ushauri kama njia ya kutatua tatizo lililomkabili. Anaenda kwa Bw. Saidi kutaka nasaha yake Bw. Saidi anamnasihi na kumweleza hatari ambazo amejiweka. Anampa ushauri apeleke mambo kwa utaratibu na ajiepushe kabisa na kosa kama hilo tena.Aidha, awe mwenye jitihada na utiifu kazini. Saidi anampa matumaini Rashid kuwa ingawa amefanya kosa, anaweza kujirudi na kuanza upya. Anamwambia kwamba ni kawaida ya binadamu kukosa hasa wakati wa ujana, anamwambia;

> '..... Binandamu yeyote hukosa, hasa wakati wa ujana. Muhimu ni kutambua kosa lako na uungwana ni kuazimia kutolirejea tena.' (Uk. 125).

Rashid, kama anavyosema mwandishi aliweza 'kutoa joto' lake kwa kuzungumzia tatizo lake. Anajiona kama aliyetua mzigo mzito aliokuwa mgongoni mwake.Alianza maisha upya kazini akiwa mchangamfu na mwaminifu kama hapo mwanzoni. Alikata kauli kutofanya kosa kama hilo tena.

4.1.2.2.2 Matumizi Mabaya ya Mamlaka

Tatizo hili la matumizi ya mamlaka lilijitokeza pia katika riwaya ya *Mali Ya Maskini* ambapo tulimwona waziri Selemani Kombo, Waziri wa Biashara ambaye alitumia nafasi yake kuwalaghai wasichana wadogo kama Zahara na kuwahamisha wengine waliompinga kama vile Yusuf. Katika *Mwisho wa Kosa*, mhusika mfano wa Selemani ni Bw.Matata ambaye alikuwa Waziri wa Elimu. Matata anatumia nafasi yake kama mheshimiwa kuwahadaa na kuwatumia wasichana wadogo. Alimhadaa Monika na kumfanya aamini kuwa angeolewa naye. Baada ya muda ndipo Monika anafumbuliwa kuhusu tabia ya Matata na wenzake kazini. Monika anahangaika sana akilini na anaamua kutafuta usaidizi kwa kwenda kwa mheshimiwa Selemani, ambaye anashirikiana na Bw.Selele na Bw.Mhaji, babake Monika ili kumnasua Monika kutoka

tatizo lililomkabili. Kadhia hii ya Monika ilijadiliwa kwa urefu hapo juu nilipojadili kuhusu kuasi utamaduni na madhara yake

Matumizi mabaya ya mamlaka ya pili ni ambapo Matata anataka kulipiza kisasi dhidi ya Rashid kwa sababu Rashid alikuwa amejaribu kumshusha moyo Monika asihusiane naye kimapenzi. Matata anampigia simu mkubwa wa Rashid, waziri mwenzake, Bw.Selemani na kumwomba amwachishe kazi Rashid mara moja. Selemani anachelea kufanya hivyo lakini kwa vile ilikuwa kawaida yao, anavyodai Matata , anafanya uovu huo shingo upande.

Baada ya Rashid kupata barua ya kuachishwa kazi kwa ghafla, anajawa na huzuni nyingi. Ilimchukua muda ili kuamini. Mwandishi anamwekea mikakati ya kujinasua kutoka mtego huo. Kwanza anapata 'kutoa joto' lake wakati ambapo analizungumzia tatizo lake na Karne, rafikiye. Karne anamliwaza na kumshauri azingatie ahadi aliyopewa na Alison, kwamba aangempa nafasi ya kazi katika kampuni yake. Rashid anamkabili waziri Selemani na kumwambia kuwa amekati kauli kutorudi tena. Alison anamnasua Rashid kutoka tatizo hili kwa kumpa nafasi ya kazi katika kampuni yake. Anampokea Rashid kwa mikono miwili, anamwambia ampelekee barua ya maombi kisha anaweza kuanza kazi mwanzo wa mwezi uliofuata. Anamwambia;

> '.Basi kwanza lete barua hiyo kesho,na halafu tarehe mosi njoo tuonane ofisini mwangu(uk209)

Rashid alifurahi sana na kumshukuru Alison kwa kumtendea hisani kwa kumpa nafasi ya kufanya kazi tena ili kujikimu maishani.Alifanya kama alivyoagizwa, akaanza kazi yake mpya na akafanikiwa sana kazini hata kuliko wakati alikuwa katika kazi ya serikali. Mwandishi katika utatuzi wa tatizo la Rashid, anampa fursa ya kuanza upya badala ya kumkatisha tamaa.

4.1.2.3 Kudhibitiwa kwa Mwanamke katika Ndoa

Burhani anatumia ndoa ya Hasani na Muna kama kielelezo cha kumulika tatizo la kunyanyaswa na kudhibitiwa kwa mwanamke katika ndoa. Engels (1884.1902) aliona ndoa kama mfumo wa ushindani ambapo wenye uwezo (wanamume) huwanyanyasa wanyonge (wanawake). Safilios (1976) anapambanua 'upendo' katika ndoa kama

sehemu ya picha ya mamlaka; mwenzi wa ndoa mwenye 'upendo' mkubwa ana mamlaka kidogo kwani yeye ni wa kumtegemea mwenzake zaidi. Ukweli wa madai ya wananadharia hawa unadhihirika katika riwaya ya *Mwisho wa Kosa*. Ndoa kati ya Hasani na Muna ilipangwa na wazee wao na hawakujuana kabla ya kula viapo vya ndoa. Salimu, babake Hasani alipeleka posa kabla ya mwanawe kurejea kutoka ng'ambo. Hasani alipofika tu harusi iliandaliwa na baada ya miezi mitatu walisherehekea harusi hiyo.

Baada ya muda mchache, Muna anaanza kulalamika kuwa hapatani na mumewe. Kwanza, hapatani naye kwa sababu hawana la kuzungumzia. Hasani hasomi chochote na hasikilizi habari ila muziki wa fujo na kutazama filamu za kitoto. Anapomlalamikia babake, anamnasihi amkubali vile alivyo na atakuja kumzoea. Pili, Hasani anamdhibiti na kumnyima uhuru wake. Hakutaka kumwona Muna akitoka na kufuatana na shogaye, Amina. Aidha, aliona wivu sana kila mara Muna alipojipamba, anampa sharti kuwa asubuhi anapotoka asijipambe akihofia atawavutia wanaume wengine. Amwambia;

> "Jambo gani linalomfanya mwanamke avalie,ajitie mapodari na marangi, ajipambe dhahabu ila kutaka kuonekana na kusifiwa na wanaume!" (uk. 188.)

Muna alijiona mtumwa katika ndoa yake, hakuwa na uhuru wa kufanya chochote bila ya ruhusa ya mumewe.

Tatu, Hasani analia ngoa ya kwamba Muna ana mshahara mkubwa kuliko wake. Wanavyosema wananadharia wa nadharia ya mgongano, Hartman (1981) na Safilios (1976) inadhihirika. Washiriki wa familia wenye mali zaidi huwa na mamlaka na uwezo wa kuamua mambo. Hasani alihofia Muna atamtawala kwa sababu ana mshahara mkubwa. Hasani anapunguza pesa zake za matumizi nyumbani kila mwezi na Muna anapolazimika kumkumbusha kuwa ni wajibu wa mme kumwangalia mke, Hasani anamwambia;

> 'Lakini unafanya kazi, unapata pesa nzuri zaidi yangu mimi'... 'Sikiliza, mimi sina pesa. Ikiwa huwezi kutumia pesa zako, basi' (uk. 198).

Kilele cha migogoro hii ya ndoa ni pale ambapo Hasani anaanza kumpiga na kumkataza Muna asiende kwao. Mambo yanapozidi, Muna anakaidi amri za Hasani na kwenda kwao. Mkutano wa dharura unaitishwa ili kuzungumzia tatizo hili na kulitatua. Baada ya mashauriano marefu, Saidi, babake Muna anamruhusu Hasani kumchukua baada ya kumpa masharti, mojawapo ikiwa ni kumruhusu atoke na awatembelee wazazi wake. Anamwambia;

> '... Lazima umpe fursa ya kutoka, kuzungumza na kuonana na wenziwe. Pia awe na ruhusa ya kuja hapa kwangu, kwa wazee wake.'

Masharti mengine kwa Hasani yalikuwa; kukidhi mahitaji yote ya Muna na kukoma tabia ya kumpiga. Hasani anamchukua mkewe na maisha yao yanaanza upya yakiwa na amani na maelewano.

Burhani ameonyesha kuwa njia ya kutatua tatizo la migogoro ya ndoa ni mashauriano na mapatano kati ya pande zote mbili. Mkosa sharti akiri kosa lake na iwe mwisho wa kosa lake. Mapatano yakifaulu maisha yanaanza upya yakiwa na imani pasi na migongano.

4.1.2.4 Wivu, Chuki na Uhasama

Burhani amelimulika tatizo la wivu na chuki ambalo linakua na kusababisha uhasama. Katika *Mwisho wa Kosa,* mwandishi ametumia wahusika Keti na Asha kuonyesha vile ambavyo wivu na chuki vinaweza kuzaa uhasama na hata kuishia vitendo vya kihalifu. Bi. Keti alitunzwa na kushughulikiwa sana na Bi. Mariyamu, mamake Asha. Asha hakufuhia hisani aliyofanyiwa Keti na mamake aliingiwa na wivu na akamchukia Keti sana. Mariyamu hakujali tabia ya Asha, aliendelea kumfadhili Keti kwani hakuwa na chochote ila uzuri wake wa sura na tabia.

Siku moja, Keti alifika kwa Bi. Mariyamu kuazima vyombo kama ilivyo desturi yake. Keti alihitaji kujipamba ili ahudhurie harusi. Bi. Mariyamu alimruhusu kuchukua vyombo hivyo. Wakati ambapo Keti alikuwa akirudisha hivyo vyombo, Asha alikuwepo nyumbani. Mariyamu alimwambia Keti avirejeshe katika kibweta bila ya kuviangalia. Asha baadaye alivichukua vyombo hivyo na kuvibadilisha na vyombo

bandia. Aliviuza vyombo vile vya dhahabu ili kulipia madeni ya mumewe ambaye alikuwa ashiki wa mchezo wa kamari. Keti anasingiziwa wizi na Asha, na anashtakiwa kwa kosa ambalo hakulitenda.

Bi. Keti anapokuwa kizuizini, anamwomba mmoja wa majirani wake amwite Bw. Mhaji, rafiki ya mumewe, Mhaji anakuwa wa msaada mkubwa kwa Keti kwani anajitolea kumlipia dhamana. Anakimbia juu chini kutafuta pesa za kumchukulia dhamana, hatimaye Bw. Selele anamkopesha na Keti anaachiliwa arejee nyumbani angojee siku ya kesi. Bi. Mariyamu anaamuakuingilia kesi hiyo kwa sababu alijua kwamba Keti hangefanya kitendo kama hicho. Anamwomba Inspekta Hamisi kesi hiyo isiende kortini kwa sababu yeye ndiye mwenye mali hiyo, Hamisi anapomwambia imekwishatoka mikononi mwake, anamwomba;

> 'Ninakuomba ufanye kila uwezavyo. Ikiwa hapana budi, Keti anaweza kuambiwa alipe thamani ya vyombo hivyo.' (uk. 28).

Kutokana na ombi la Mariyamu, kesi inapofanywa, Keti anaachiliwa na kutakiwa alipe thamani ya mali hiyo.

Miaka kadhaa baadaye wakati Mariyamu alianza kuugua, anamwita Keti na kumwomba msamaha kwa makosa ya mwanawe na kumfidia kwa kumpa pesa na kumgawia mali katika wasia wake. Baada ya Mariyamu kuaga dunia, Inspekta Hamisi anachukua hatua kuitisha mkutano wa kupatanisha Keti na familia ya marehemu Mariyamu na kumpa Keti haki yake aliyoachiwa na marehemu; pesa na nyumba. Keti anapata kupumzika baada ya kuhangaika kwa muda. Tatizo lililomkabili linafikia tamati.

Kupitia kadhia za Bi. Keti, mwandishi anadhihirisha umuhimu wa utu na kwamba haki ya mtu haipotei. Tunaona moyo wa kujitolea kupitia kwa wahusika kama vile Bw. Mhaji na Bw. Selele. Bi. Mariyamu anapotambua ukweli kuwa ni Asha aliyehusika, anachukua hatua ya haraka kumwomba msamaha Bi. Keti na kumfidia. Hatua hii inarudisha amani iliyokwepo hapo awali kabla ya wizi wa mali ya Mariyamu. Mwisho wa kosa unapofika, maisha yenye maelewano yanaanza tena kati ya familia hizo mbili zilizokuwa katika mgongano.

4.2 Namna Burhani Anavyotatua Matatizo Hayo

Baada ya kuchanganua matatizo mbalimbali ambayo Burhani anayamulika katika riwaya zake, kumedhihirika namna anavyotatua matatizo hayo, tunaweza kumkadiria na kumtuza kwa kufaulu kutekeleza wajibu wake kama msanii anayetaka jamii yake iwe bora na yenye salama na amani zaidi. Burhani amefaulu katika kumulika matatizo ambayo ni yakinifu na yanayodhihirika katika jamii ya Afrika Mashariki ya leo. Kadhia za kifisadi kama vile ulaji rushwa, na matumizi mabaya ya mamlaka ni masuala ambayo huzungumziwa kila mara katika vyombo vya habari. Mengine yanayojitokeza katika mahusiano ya kijamii katika maisha ya kila siku, kama vile chuki, wivu na anasa

Katika uchanganuzi, imedhihirika kuwa Burhani ametumia mbinu ya kiliberali (ushauri), mbinu hii inaoana na mikakati iliyopendekezwa na Stein et al (1992) ilivyojadiliwa katika misingi ya kinadharia-2.3 katika sura ya pili. Mikakati ya utatuzi iliyopendekezwa na Stein et al ni; ukaribishaji, mapatano, na kuondoa migongano kiitikadi. Mikakati aliyopendekeza Burhani ni inayoleta mapatano na kurejesha hali ya salama na amani katika maisha ya jamii kama ilivyo hapo awali. Burhani katika kufanya hivyo anatumia mikakati ifuatayo:

4.2.1 Kutambua Tatizo

Hatua ya awali katika utatuzi ni wakati ambapo, mhusika anapewa nafasi ya kutambua kosa lake ama anavyoathiriwa na tatizo. Mkakati huu haukurejelewa katika nadharia ya mgongano. Baada ya huo utambuzi, hatua zingine za kulitatua tatizo zinafuata. Mathalani, katika *Mali ya Maskini*, Kadiri anatambua tatizo lake la umaskini ambalo lilimwelemea yeye na aila yake, anaanza kutafuta njia ya kujinasua kwa kuzingatia mikakati mingine aliyowekewa na mwandishi. Tatizo la Ali linapozidi na Kadiri kufichuliwa kuhusu upotofu wa mwanawe, kuwa amefikia kiwango cha kujihusisha na magendo ili kukidhi tamaa za Keti, anatambua kuwa kuna tatizo na ananza kuchukua hatua ili kumnasua mwanawe kutoka tatizo hilo.

Zahara anapoona waziri Selemani ana mipango mibaya kwake, anatambua kuwa kuna tatizo na anaanza kuchukua hatua za kujinasua kutoka hila za mzee huyo. Zahara angekosa kutambua hila za Selemani, labda hangepata fursa ya kuolewa na kipenzi chake Yusuf.Mkakati huu unaonekana tena ambapo Zahara anachukiwa sana na mke wa Bakari, Imani. Zahara anatambua kuwa kuna tatizo na anachukua tahadhari asije akazusha zogo kati yao.

Ali pia anapoonywa dhidi ya kijiingiza katika shughuli za magendo, anatambua kuwa kuna tatizo na anakoma mara moja kazi yake ya kusafirisha bidhaa za magendo kila mwishoni mwa wiki. Ingetokea kuwa Ali asitambue tatizo hilo, labda angepata hukumu ya kifungo cha miaka mingi ama hata kunyongwa

Katika *Mwisho wa Kosa*, Bi.Mariyamu anapogundua kuwa aila yake imemkosea Bi.Keti kwa kumtuhumu bure, anatambua kosa lake na linakuwa mwanzo wa utatuzi wa tatizo lililomkabili Bi Keti, anaamua kumfidia Keti kwa kumpa nyumba na pesa kwa hasara aliyomtia muda wote alipokuwa akimlipa pesa kila mwezi kwa mali ambayo hakuiba. Monika anapofumbuliwa ukweli kuhusu tabia na hila za Bw. Matata, anatambua kuwa kuna tatizo na anachukua hatua mara moja kutafuta usaidizi kutoka wahusika wengine. Ali anapofukuzwa kutoka shule, aila yake, marafiki na yeye mwenyewe wanatambua kuwa kuna tatizo na wanachukua hatua kutafuta suluhisho. Rashid anaponaswa katika utando wa ulaji rushwa, uvumi unaoenea ofisini unamfikia na anatambua kuwa kuna tatizo na anachukua hatua mara moja kutafuta ushauri kutoka mzee aliyemwamini. Mifano ya wahusika wanaotambua makosa yao ni wengi, kwa hivyo hatua ya utambuzi wa tatizo ama kosa ni mkakati wa kwanza ambao Burhani anapendekeza utumiwe.

4.2.2 Kulizungumzia Tatizo

Hatua ya pili ni wakati ambapo, mhusika aliyeathiriwa anapewa nafasi na mwandishi kuzungumzia tatizo na mtu mwingine ili 'kutoa joto' lake la moyoni juu ya athari ya tatizo hilo. Mkakati huu pia haukupendekezwa katika misingi ya nadharia. Ni njia iliyowapoza waathiriwa wengi sana na kuwafanya wajisikie kama kwamba wametuliwa mzigo mkubwa, anavyosema Burhani, 'kutoa joto' lao. Kwa mfano, katika

Mwisho wa Kosa, Muna anapomwendea Ali ili kuzungumzia tatizo lake la kunyanyaswa na mumewe, baada ya kufanya hivyo Muna anaona nafuu kidogo na safari ya utatuzi wa tatizo lake inaanza. Ali anapofukuzwa kutoka chuoni, alipoamua kwenda kwa babake kuzungumzia tatizo lake, anajisikia kama aliyetulishwa mzigo mzito.

Monika naye anapojikuta katika hali ya mtafaruku baada ya kufumbuliwa macho na wenzake kazini kwa kufichuliwa ukweli kuhusu hila za Bw. Matata, anamkimbilia Bw. Selemani ili apate 'kutoa joto' lake la motoni na kuhakikishiwa ukweli wa habari aliyopata. Mzee huyo alimposa na kumsaidia katika safari yake ya kutatua tatizo hilo kikamilifu. Rashid kwa upande wake anamwendea Bw.Saidi ili kutoa 'joto lake' baada ya kujikuta amenaswa na utando wa ulaji rushwa na alikuwa katika hatari ya kupoteza kazi yake na hata kushtakiwa. Baada ya kumwelezea mzee huyo tatizo lake, anapata ushauri wa kumfaa kuhusu jinssi ya kulikabili tatizo hilo.

Katika *Mali ya Maskini*, Kadiri anamgombeza mkewe baada ya kufilisika na kuelemewa na tatizo la umaskini, mkewe hakulalamika kwa sababu alielewa kuwa Kadiri alihitaji sana 'kutoa joto' lake ili aweze kurejea hali yake ya kawaida. Zahara kwa upande wake anamtafuta Yusuf ili 'kutoa joto' lake kuhusu sarakasi za Selemani, mkubwa wake kazini. Zahara kila mara aliposumbuliwa na hila za Selemani alimwendea Yusuf kutafuta kutulishwa mzigo wake. Alama kwa upande wake anamwendea mamake baada ya kunyanyaswa na Ali na kugundua kuwa uhusiano wake na Keti haukuisha japo alikuwa amemwoa, anapata kutoa joto lake na mamake anampa nasaha kuhusu maisha ya ndoa na jinsi anavyohitajika kuvumilia.

4.2.3 Kustahimili

Hatua ya tatu ni mhusika aliyeathiriwa kustahimili wakati tatizo linatokea na utatuzi wake haujakamilika. Mkakati huu pia haukujitokeza katika misingi ya nadharia. Mkakati huu ulikuwa ni njia iliyotumika ili kupunguza uwezekano wa kutokea ugomvi na vita kati ya wanaohusika. Kwa mfano, katika *Mali ya Maskini,* Zahara anapochukiwa na kuteswa na Imani, mke wa Bakari, ami yake, Zahara alipogundua kuwa Imani alimchukulia sana, alivumilia na kutafuta njia za kuepusha zogo kati yake na Imani.

Alianza kufanya masomo yake kwa rafikize na maktabani ili kupunguza muda wake pale nyumbani.

Katika *Mwisho wa Kosa,* Ali analazimika kustahimili baada ya kufukuzwa kutoka chuoni, anavumilia, anakukubali kufanya vibarua ili kujitafutia nafuu. Wakati mmoja alifanya kazi ya kuandika makala katika gazeti, kazi ambayo haikumtosheleza kwa sababu hakupewa nafasi ya kutosha katika gazeti lile. Ali aliendelea kuvumilia mpaka pale ambapo anapata kazi katika kampuni moja ya Alison. Bi. Keti naye ni mhusika aliyeonyesha usthimilifu sana. Baada ya kutuhumiwa kuwa aliiba mali ya Bi. Mariyamu na kuamuriwa na mahakama alipe thamani ya mali hiyo, alivumilia na kujikakamua kulipa japo uwezo wake kifedha ulikuwa wa chini. Keti aliendelea hadi pale ambapo Bi. Mariyamu anatambua ukweli na anaamua kumfidia Keti.

Muna naye ni mhusika ambaye alivumilia mateso katika ndoa. Mumewe, Hasani alimdhibiti kwa kumzuilia asiende kwao na kutomruhusu avae anavyotaka. Aidha alifikia kiwango cha kumpiga, hapo ndipo Muna aliona amevumilia vya kutosha na anaamua kurudi kwao ili mashauriano yafanywe. Muna angekosa ustahimilivu, labda ndoa yake na Hasani haingedumu.

4.2.4 Mashauriano na Mapatano

Hatua ya nne ni kushauriana na kupatana hasa baina ya wazee miongoni mwa washiriki wa familia na marafiki ili kubadilishana mawazo na kutafuta suluhisho kwa pamoja. Mkakati huu ulirejelewa katika mikakati aliyopendekeza Stein et al (1992), mkakati alioutumia Burhani ni kama kujumlilishwa kwa mikakati yote mitatu iliyopendekezwa na hawa wanasosiolojia; ukaribishaji, upatanisho na kuondoa migingano kiitikadi.

Familia ya Kadiri katika *Mali ya Maskini* inachukua hatua na kutumia mkakati huu wakati ambapo wanagundua kuwa Ali amekengeuka na kupotoka. Wanashauriana na kuazimia kumwoza mke, Alama. Mfano mwingine ni wakati ambapo waziri Selemani anapeleka posa kwa rafikiye Kadiri, kutaka kumposa Zuhura, Kadiri anashindwa kumkataa moja kwa moja na anaamua kuitisha mkutano wa wazee wa aila

yake ili washauriane, pia wanamshauri Zahara ili kusikia msimamo wake. Baada ya kufanya mashauriano hayo, Kadiri anapata nguvu ya kukataa posa ya Selemani kwa wepesi, kwamba uamuzi ni wa wazee na Zahara mwenyewe bali si wake.

Katika *Mwisho wa Kosa*, mkutano unaitishwa baina ya aila ya Hasani na ya Muna ili kutafuta suluhisho la ndoa yao iliyokuwa na tatizo. Mashauriano na mapatano yanafanywa na Bw. Saidi, babake Muna, anampa masharti Hasani kabla ya kumchukua mkewe, masharti ambayo Hasani na aila yake wanakubali. Mfano mwingine ni wakati ambapo Monika anaingiwa na mtafaruku baada ya kufichuliwa ukweli kuhusu ujanja wa Bw. Matata. Bw. Mhaji anashauriana na wazee wenzake kama vile Selele na Selemani. Baada ya mashauriano. Mhaji anakubali kumrejesha Monika nyumbani kwa sharti moja, kuwa Monika aozwe pindi Mume atokeapo. Hatimaye, Monika anaozwa kwa Shaaban na anaanza maisha upya kama mke wa mtu.

4.2.5 Kufaana na Kufadhiliana

Hatua ya tano ni kufaana na kufadhiliana, yaani kujitokeza na kujitolea wakati ambapo mshiriki mmoja wa jamii alihitaji msaada wa namna fulani. Mkakati huu haukurejelewa katika misingi ya nadharia. Mkakati huu ni njia iliyotumiwa sana katika riwaya za Burhani. Kwa mfano, katika *Mali ya Maskini,* Hasani alipotoa pesa zake ili kumfaa rafiki yake Kadiri wakati ambapo alikuwa amelemewa na umaskini na kuweza kumnasua kutoka tatizo hilo, Kadiri alikuwa atumie pesa alizopewa na rafikiye kufanyia biashara kisha wagawane faida nusu bin nusu. Mfano mwingine ni usaidizi alioutoa Bakari ili kumsaidia Kadiri wakati ambapo alikuwa amefilisika, anajitolea kuwakimu wanawe wawili; Ali na Zahara kwa kuwalipia karo na kumchukua Zahara akakae kwake, aidha alimpa Ali mafunzo ya ufundi baada ya shule.

Katika *Mwisho wa Kosa*, Alison anamfadhili Rashid baada ya kuachishwa kazi. Anampa kazi katika kampuni yake ya utengenezaji wa magari. Rashid anafanikiwa sana hata anapata fursa ya kwenda ng'ambo kuongeza ujuzi wake wa kazi. Mfano mwingine ni wakati ambapo Karne anajitokeza na kumfadhili Ali kwa kumsaidia kupata kazi katika gazeti moja ya kuandika makala. Baadaye, Ali anabahatika zaidi na kupata kazi katika kampuni ya Alison. Selele kwa upande wake anajitolea kumlipia Monika kodi

ya nyumba ambayo Matata alikuwa amekwepa kulipa baada ya kumhadaa Monika. Mwisho, Mhaji alijitolea kumchukulia Bi.Keti dhamana baada ya kutiwa nguvuni kwa tuhuma za Asha kuwa aliiba mali ya mamake.

4.2.6 Asasi za Jela na Mahakama

Asasi za jela na mahakama zilitumika wakati ambapo mikakati yote iliyotajwa hapo juu ilikosa kufaulu. Mkakati huu haukurejelewa pia katika misingi ya nadharia. Katika hatua hii, wakosa walitiwa nguvuni na kushtakiwa. Kwa mfano, Ali alipokaidi juhudi za aila yake na marafiki katika *Mali ya Maskini*, alitiwa nguvuni na kushtakiwa kwa kosa la kumuumiza Keti na alipoachiliwa huru alikiri makosa yake na kuahidi kutorudia tena. Ali aliamuriwa na mahakama amlipe Keti hasara yote aliyopata. Kufungwa jela kulimsaidia Ali kwani baada ya hapo, alifunguka macho na akaahidi katohusiana na Keti tena, anaamua kuishi na mkewe na kuwa mwaminifu.

Katika *Mwisho wa Kosa*, Bi.Keti anafikishwa mahakamani baada ya Asha kumtuhumu na kumsingizia wizi, hata hivyo, njia hiyo haikutimia kwa sababu Bi, Mariyamu aliingilia kati. Badala ya Keti kuhukumiwa, anaamuriwa awe akilipa shilingi elfu moja kila mwezi hadi atakapomaliza thamani ya mali ya Bi. Mariyamu. Baada ya Mariyamu kugundua njama za mwanawe Asha za kumsingizia Keti kosa ambalo hakulitenda, anamfidia Bi, Keti.

Kutokana na mikakati hiyo iliyotajwa hapo juu, Burhani anajitokeza kama msanii anayewapa wahusika wake njia na nafasi ya kujirudi na kuanza upya maisha yao. Hata hivyo, mbinu ya kiliberali (ushauri) aliyotumia Burhani kutatua matatizo haikufaulu sana kwa sababu imeegemea upande mmoja; upande wa watu wa kawaida. Burhani hakuwachukulia hatua yoyote wahusika wenye uwezo mkubwa kama vile mawaziri na matajiri. Mawaziri kama vile Matata, Selemani Kombo na Selemani wa *Mwisho wa Kosa* walifanya maovu na hatukuwaona wakishauriwa wala kukiri uovu wao.

Matajiri kama vile Asha bintiye Bi Mariyamu ambaye alimtuhumu Bi. Keti hakushauriwa na yeyote, Alison ambaye alishiriki katika ulaji rushwa hakushauriwa pia.

Kwa hivyo, inaweza kudaiwa kuwa Burhani ni mwandishi anayewapendelea wanajamii wenye uwezo mkubwa ama anachukulia uovu wautendao kuwa si tatizo.

SURA YA TANO

HITIMISHO

5.0 Utangulizi

Katika utafiti huu, nilichanganua riwaya za Burhani: *Mali ya Maskini* na *Mwisho wa Kosa.* Nimefanikiwa kuchanganua matatizo mbalimbali yaliyomulikwa na namna ambavyo Burhani anatatua matatizo hayo. Kwanza, nilipambanua matatizo yaliyomulikwa katika riwaya hizo kisha mikakati ambayo mwandishi ametumia katika utatuzi wa matatizo hayo.

Utafiti ulitumia nadharia ya mgongano ambayo iliasisiwa na Karl Marx, mtazamo wa wanasosiolojia. Nadharia hii inahusu migongano katika nyanja mbalimbali katika jamii, kisha inapendekeza njia za kuondoa matatizo yanayotokana na migongano hiyo. Burhani katika riwaya zake ameyamulika matatizo mbalimbali katika jamii ambayo yanaibusha migongano; migongano ambayo inapofikia kilele, mwandishi anaweka mikakati ambayo wahusika wanaitumia ili kuondoa matatizo hayo. Utafiti ulitumia utaratibu wa upekuzi wa yaliyomo katika ukusanyaji wa deta na mbinu ya kithamano katika uchanganuzi wa deta. Utafiti ulifanikiwa kupata matokeo ambayo yaliweza kuthibitisha nadharia tete zote za utafiti.

5.1 Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti yaliweza kuthibitisha nadharia tete za utafiti. Kwanza ni kwamba, Burhani ameyamulika matatizo mbalimbali yanayokabili jamii, hakujifunga katika tatizo moja. Matokeo yamedhihirisha kwamba, Burhani hakujifunga katika tatizo moja mahsusi, bali amegusia takribani kila nyanja ya maisha. Mathalani; mkengeuko wivu, chuki, uhalifu, ndoa siasa, uchumi, ufisadi miongoni mwa masuala mengine. Pili ni kwamba, Burhani ametumia mikakati mbalimbali katika utatuzi wa matatizo aliyoyamulika katika riwaya zake. Matokeo ya utafiti yameweza kuthibitisha kwamba, Burhani amewawekea wahusika wake mikakati mbalimbali, hasa ya kiliberali, ambayo inahimiza mashuriano na mapatano, Mikakati hii inawasaidia katika utatuzi wa matatizo yaliyowakabili.

Deta ya utafiti huu ilikuwa ni matukio yanayodhihirisha matatizo mbalimbali na juhudi za wahusika katika kuondoa matatizo hayo kwa kutumia mikakati ambayo mwandishi amewawekea. Katika *Mali ya Maskini,* anayoyamulika ni: umaskini, chuki, matumizi mabaya ya mamlaka na mkengeuko wa vijana. Matatizo haya yanakua na kufikia kilele ambapo suluhisho linaanza kutafutwa. Katika *Mwisho wa Kosa,* anamulika matatizo kama vile; mkengeuko, kudhibitiwa kwa mke katika ndoa, ulaji rushwa, wivu, chuki na uhasama na matumizi mabaya ya mamlaka. Hali kadhalika, mwandishi anaweka mikakati mbalimbali ili kuondoa na kutatua matatizo hayo. Katika vitabu hivi viwili, Burhani anawawekea wahusika mikakati ya kutumia ili kupunguza na hatimaye kuondoa matatizo hayo. Kwanza anapendekeza anayeathiriwa atambue tatizo ama kosa lake, kisha alizungumzie na mtu anayemwamini ili 'kutoa joto' lake la moyoni. Mikakati mingine ni ustahamilifu, mashauriano na mapatano yanafanywa. Mikakati hiyo isipofaulu, anapendekeza asasi za jela na mahakama zitumiwe.

Ilidhihirika kwamba, Burhani amefanikiwa kutatua matatizo yanayoibuka katika mahusiano ya kijamii kwa njia ambayo haihasiri mhusika yeyote bali inaleta mapatano na kuwapa wenye kosa na waathiriwa fursa ya kuanza upya. Burhani ni mwandishi anayewapa wahusika wake matumaini tofauti na waandishi wengine kama vile E. Kezilahabi ambaye suluhisho analotoa ni la utamaushi, wakati mwingi, matatizo yanayomkabili mhusika yanapofikia kilele, suluhisho linakuwa mauti. Mathalani, Rosa katika *Rosa Mistika.*

Kama wazo la ziada, ilibainika pia kwamba Burhani alijiepusha na masuala nyeti ya siasa. Mara chache alipowaangazia viongozi wa kisiasa aliwamulika katika maingiliano yao kijamii na umma. Hata hivyo, wanasiasa hawa wakati mwingi wanajitokeza kama wenye tabia mbovu. Mathalani Bw. Selemani katika *Mali ya Maskini* na Bw. Matata na Bw. Selemani katika *Mwisho wa Kosa.*

Burhani kama mshiriki wa jamii ya Kiafrika amemulika matatizo ambayo ni yakinifu katika jamii ya Kiafrika ya kisasa. Matatizo kama vile, mkengeuko, kudhibitiwa kwa mwanamke katika ndoa, madawa ya kulevya na ufisadi ni mambo

ambayo yanaripotiwa kila siku katika vyombo vya habari nchini Kenya na ulimwenguni kote.

Mwisho, Burhani amefanikiwa kuhitimisha dhamira yake kuu ya kutoa mafunzo kwa vijana ambao wanahangaishwa na ujana na utamaduni wa kigeni. Vijana wanaonyeshwa umuhimu wa kurudi nafsi zao baada ya kupotoka ili waongoke. Aidha watafute ushauri kutoka kwa wazee wenye busara ili wapate mwelekeo mwema maishani.

5.2 Matatizo Yaliyokumba Utafiti

Utafiti huu haukukabiliwa na matatizo makubwa. Jambo ambalo lilitatiza tu ni ugumu niliopata katika kutafuta habari kuhusu mwandishi, sikuweza kupata habari zozote kuhusu wasifu wa Burhani na mazingira aliyokulia. Habari hizo zingepatikana, utafiti ungefaidika kwa kuweza kuhusisha matokeo ya utafiti na wasifu wake mwandishi. Wachapishaji wa riwaya hizi; Longhorn hawakutoa habari zozote kuhusu mwandishi kama wanavyofanya katika jalada za riwaya zingine.

5.3 Mapendekezo

Riwaya za Burhani hazijatafitiwa zaidi kama riwaya zingine za Kiswahili. Utafiti huu umejikita tu katika baadhi ya maudhui. Kuna sehemu nyingi katika riwaya hizi zinazohitaji utafiti. Mathalani, wahusika na uhusika, suala la umenke, mbinu za uandishi na kadhalika. Watafiti wa siku zijazo wanaweza kuchukua mada mojawapo na kutafitia. Pili waandishi wa riwaya waandike riwaya zao wakiwafikiria wanajamii, riwaya wanazotunga zitawafaa kwa njia gani? Iwe ni kazi ambayo inamulika uhalisia, inayojadili matatizo katika jamii na kupendekeza njia nzuri za kuwarudi wale wakosa na kuwawezesha kuanza upya, namna ambavyo, Burhani anafanya.

MAREJELEO

Achebe C (1974) *Arrow of God.* London Heinman

Burhani Z (1981) *Mali ya Maskini.* Hong Kong Longman

_____ (1987) *Mwisho wa Kosa.* Kenya Longman

Crystal D (1987) *The Cambridge Encyclopaedia of Language.*C.U.P New York

Eldred D. J (1979) *African Literature Today 10 Retrospect and Prospect.* Nairobi Heinnman

Forster E.M (1982) *Aspects of the Novel.* Edited by Stllybrass O. England. Penguin Books Ltd.

Global Encyclopedia (1991) Vol 5. Alexandria, Virginia. Lexicon Publications

Held D (1980) *Introduction to Critical Theory.* Horkheimer to Habermas. Polity Press. U.S.A

Izevbaye D (1979) *The African Novel* katika Eldred D (1979) *African Literature Today* 10 Retrospect and Prospect.Heinnman Educational books.Nairobi.

Hussein E.N (1971) *Wakati Ukuta.* Nairobi E.A.P.H

_____ (1971) *Mashetani.* Nairobi/ Dar es Salaam. OUP

Kamunde M.E (1983) *Kilio Cha Wanyonge* katika Riwaya za S.A Mohamed.Nairobi:Tasnifu ya MA. Chuo Kikuu Cha Nairobi

Kezilahabi E (1971) *Rosa Mistika.* E,A,P. Arusha.

_____(1975) *Dunia Uwanja wa Fujo.* E.A.P. Arusha

Kiswahili (1986) Tuki, Juzuu 53/1 na 53/2. Wajariri: Mulokosi Massamba.

Lewis C.A (1956) *The Functions of Social Conflict.* NewYork . Free Press

Macmillan English Dictionary for Advanced Learners (2002) Nairobi. Macmillan

Mazrui A. (1984) *`Uhakiki wa Dunia Mti Mkavu'*,Katika *Kiswahili* Vol.51/1,52/1 Jarida la *TUKI.* Dar es Salaam Chuo kikuu cha Dar es Salaam

Marx K na Engels F (1973) *On Literature and Art*. International General. NewYork.

Mohamed S.A (1980) *Dunia Mti Mkavu*. Nairobi . Longman

_____ (1977) *Asali Chungu*. Nairobi E.A.E.P.

_____ (1980) *Utengano*. Nairobi . Longman

Mkangi K (1995) *Walenisi*. Nairobi . E.A.E.P

Mlacha S.A.K (1985) '*Riwaya za Visiwani (1970-1880) na Ujenzi wa Jamii Mpya*' katika *Mulika Na. 16*. Jarida la TUKI (1985) Dar es Salaam:Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

_____ (1986) *The Identification of Personality Difference In Kiswahili Prose Fiction* Katika *Kiswahili*, Jarida la TUKI, Juzuu 53/1 na 53/2 (1986). Wahariri: M.M Mulokosi na D.P.B Massamba.

Msokile M (1993) *Msingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi . E.A.E.P

Mugenda O.N na Mugenda A.G (1999) *Research Methods Quantitative and Qualitative Approaches*. Nairobi. Act's Press.

Mulika 17 (1985) Edited by Mdee J.S and TUKI . Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Ngara E (1982) *Stylistic Criticism and the African Novel*. London. Heinman

Ngugi wa Thiongo (1982) *Shetani Msalabani*. Nairobi. Heinman.

_____ (1981) *Writers in Politics*. Nairobi. Heinman

_____ (1986) *Decolonizing the Mind*: *The Politics of language in African Literature*. London . James Currey Ltd.

Njogu K (1997) *Uhakiki wa Riwaya za Visiwani Zanziba*. Kenya. Nairobi University press.

Njogu K na Chimerah, R (1999) *Ufundishaji wa Fasihi*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Roger F (1977) *Structuralism and Post Structuralism* katika *Modern Literary theory,* A comperative Study. Edited by Jefferson A and David R (1982) Batsford Ltd. London.

Senkoro F.E.M.K (1982) *Fasihi.* Dar es Salaam. Press and Publicity Centre.

Shabaan Robert (1951) *Kusadikika.* Nairobi. Evans Brothers.

_____ (1951) *Adili na Nduguze*. London. Macmillan

Shafi S. A (1978) *Kasri ya Mwinyi Fuad*. Dar es Salaam. Tanzania Publishing House.

Shija A.N (1975) *Wahusika wa Shaaban Robert* Katika *Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili.* (1975) Mhariri: Topan M.F. O.U.P Dar es Salaam.

Stein J.P et al (1992) *Sociology* : Brief Edition NewYork Macmillan

Smelser J.N (1991) *Sociology* : *A Division of Simon and Schuster*. New Jersey Eaglewed Cliffs.

Topan F.M (1975) *Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili*.Dar es Salaam. OUP

_____ (1977) *Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili*.Dar es Salaam. OUP

Todorov T (1977) *Theories Du Symbole*.Translated Cuthrine Porter(1982),Basil Blackell

Thurston T (1947) *Multiple Factor Analysis*. University Press. Chicago.

Vuzo M.A (1999) *Mwongozo wa Siku Njema*. Nairobi. Macmillan

Wamitila K.W (2000) *Uhakiki wa Fasihi*: *Misingi na Vipenge Vyake*. Nairobi. UON

_____ (2003) *Mwongozo wa Walenisi*. Nairobi. Sema Sema Publications.

Zanden V.J Wilfrid (1988) *The Social Experience. An Introduction to Sociology*. NewYork. Random House

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY